# *Kujaribu Kumtumikia Mungu Bila ya Kuwa Ni Mapenzi ya Mungu*

Ndugu wahudumu, nanyi marafiki huko nje, ninasema ni majaliwa kuwa hapa asubuhi ya leo. Utambulisho wa namna hiyo, mbona, sijui nitaishije kamwe kuustahili.

2 Lakini nilipokuwa nimeketi tu pale nikizungumza, mimi na Ndugu Noel, siamini nimewahi kukutana na mtu ambaye hasa ni...Sote tumefanywa katika miundo tofauti, lakini na Mungu yeye yule. Kama tu vile Ndugu Jack Moore, bila shaka amekuwa... Ndugu Noel alikuwa tu akisema, "Tangu nimekuwa hapa pamoja naye..." Huyo ni mkwewe, na jinsi alivyojifunza kumpenda na kuheshimu hekima yake na kadhalika. Na kwamba...Ninaweza kusema "amina" kwa jambo hilo. Mambo mengi mazuri...wakati ambao tumekuwa pamoja naye, mimi na yeye, na Ndugu Brown, Ndugu Bootlayer hapa. Watu wazuri wa Mungu ambao kweli ninawapenda kwa moyo wangu wote.

3 Na sasa ninaona hatuwi vijana kamwe, ama nafikiria tu juu ya wakati sasa ambapo tunajiona tunapobadilika tangu yapata miaka ishirini iliyopita tulipokuwa tukivuka majangwa, na kadhalika pamoja kama vijana. Lakini kujua tu ya kwamba kuna Nchi ambapo hatutazeeka kamwe. Tutakutana kule tena siku moja.

4 Jana usiku nilipokuwa nikiondoka maskanini, kulikuwako na maskini bibi mmoja amelala kule kwenye machela, naye alisema, "Ndugu Branham, miaka kadha iliyopita..." Nafikiri alikuwa amelemaa. Kasema, "Uliniambia..." Ninasahau alilosema mwanamke huyo sasa, kitu kama hiki, ninatumaini ya kwamba sitalinukuu vibaya. Kasema, "Ya kwamba mateso haya niliyokuwa nayo yalikuwa ni kwa kusudi fulani," ama kitu fulani, ya kwamba angemzaa mtoto. Naye hangeweza kufahamu jinsi ambavyo hilo lingetendeka naye yumo katika hali kama hiyo.

5 Hapo alisimama kijana mwanamume mdogo, anayependeza, akasema, "Mimi ndimi mtoto mchanga ambaye alimzaa." Akasema, "Mimi ndimi mtoto huyo mdogo aliyemzaa."

6 Na mambo mengi sana yametendeka njiani, hata hatuna wakati hapa wa kuzungumzia jambo hilo. Tutalizungumzia kwenye ng'ambo ya pili.

7 Na Tawi hili la Wafanyi Biashara. Mimi si mfuasi wa shirika lo lote, nadhani nyote mnajua, lakini mimi . . . Hili ndilo kundi peke yake ambalo mimi nina uhusiano nalo, ambalo nina kadi yake ya ushirika, ni . . . Wao ni wa baina ya madhehebu, ni wafanyi biashara tu. Wamekuwa faida sana kwangu na kwa huduma ambayo Bwana Baba yetu amenipa mimi. Ni . . . si kwamba mimi sipendi madhehebu; ni huduma tu ambayo nimepewa, na kama mimi si mwaminifu kwa wito huo, basi nitakuwa mtu asiye mwaminifu kwa Mungu.

8 Na, ninafikiri, kabla tu sijatoka Tucson, labda wengi wenu mlikuwa huko, siku moja nilikuwa huko Los Angeles nikizungumzia tawi hilo. Na kulikuwako na . . . Ndiyo kwanza ki—kidogo niyakemee madhehebu labda sana. Si— sikumaanisha kuwa namna hiyo. Kama ulitaka hilo liwe duni, basi ningekuwa mnafiki. Haikupasi kufanya jambo hilo, la, hilo linamtupilia mbali mtu fulani. Lakini nilikuwa nimezungumza juu ya mti ambao niliuona kwenye ua la Ndugu Sharrit. Ulikuwa na aina kama tano mbalimbali za matunda. Ndipo nikasema, "Sijapata kuona mti kama huo maishani mwangu." Ulikuwa ni . . . ulikuwa na mabalungi, ulikuwa na malimau, ulikuwa na chenza, kangaja, machungwa, kila kitu kikikua juu ya mti ule ule. "Vema, nikasema, hakika sifahamu jambo hilo. Kwani ni mti wa aina gani huu?"

"Ni mchungwa."

Nami nikasema, "Vema, zile ni balungi?"

Kasema, "Naam."

Ni—nikasema, "Yawezekanaje?"

Kasema, "Huo umepandikizwa."

Ndipo nikasema, "Loo, sawa."

9 Akasema, "Yote ni jamii ya mchungwa, na mti wo wote ulio wa jamii ya mchungwa unaweza . . . unaweza kupandikizwa."

10 Nikasema, "Nafahamu." Ndipo nikaaza kupiga makelele kidogo tu, mwajua, maana mimi ni mtu mwenye wasiwasi na mwenye mhemko.

11 Kwa hiyo, akasema, "Kuna nini?"

12 Ndipo nikasema, "Vema, nilikuwa nikiwazia tu juu ya jambo fulani." Kisha nikasema, "Sasa ninataka kukuuliza swali." Nikasema, "Sasa, mwaka ujao wakati wa kuchanua, hakutakuwako na machungwa, makangaja, mabalungi, malimau; kutakuwako tu na machungwa kwa sababu huo ni mchungwa, sivyo?"

13 Akasema, "La, la. La, kila tawi linazaa kwa jinsi yake."

14 Kasema, "Sawa."

15 Kwa hiyo hilo bado lilikuwa linasikika zuri sana, kwa sababu mimi . . . mwajua mimi ni . . . bila shaka nina digrii kutoka

Hartford na vyuo hivi vingine vyote, mwajua. Kwa hiyo—kwa hiyo mimi . . . angalia *viumbe*, hayo ndiyo chuo kikuu kilicho bora kuliko vyote nilivyopata kuona bado, chuo kikuu cha Muumba. Kwa hiyo mimi hungalia hivyo, ninapata mahubiri yangu kutokana na vile ninavyoona viumbe vikitenda.

16 Ndipo nikasema, "Vema, hilo linanifanya tu mimi kujisikia vizuri sana."

17 Akasema, "Kuna nini?"

18 Nikasema, "Niliwazia tu jambo fulani."

19 Kwa hiyo, siku hiyo, nilikuwa nikihubiri juu ya jambo hilo. Nikasema, "Sasa, mnaona, wakati kanisa lilipoanza mara ya kwanza, lilikuwa . . . Yesu alisema . . . " Nilikuwa nikihubiri Yohana 15. "'Mimi Ndimi Mzabibu, ninyi ni matawi. Na kila tawi lisilozaa tunda litakatwa, lichomwe.'"

20 Na mtu fulani yuko tu kooni mwangu akinikaba sana kwa ajili ya jambo hilo, kasema, "Unaona, nilifikiri kama kweli wakati mmoja ulikuwa umejazwa na Roho Mtakatifu na umeokolewa, ulisema, 'hawangeweza kuliepa jambo hilo.'"

21 "Hiyo ni kweli."

22 Akasema, "Na *hilo* je?

23 Nikasema, "Sasa unazungumzia jamo lingine. Yeye anazungumza juu ya kuzaa matunda pale, si Mzabibu; anazungumzia juu ya kuzaa tunda, wala si Uhai. Akasema, 'Vema, ukate tu mti upate kukua, kuzaa tunda.'"

24 Akasema . . .

25 Ndipo nikasema, "Sasa, unaona, mti huu, ulipoanza, wote ulikuwa ni halisi, Wakristo wa Biblia. Ndipo likatokea tawi linaloitwa Luther, na Methodist, Batisti, Presbiteri: malimau na kadhalika." Kisha nikasema, "Unaona, unastawi kwa jina la Ukristo, lakini una- . . . Unaishi kwa kutegemea Mti ule, lakini unazaa ya jinsi ya madhehebu yake. Unaona? Lakini" nikasema "kama mchungwa huo ukiwahi kutoa tawi lingine wenyewe, utazaa machungwa kama ulivyofanya hapo mwanzo."

26 Kwa hiyo huo ni yule mtu anayeketi pale, kiongozi wa ninii kubwa . . . moja ya madhehebu yaliyo makubwa sana ya Kipentekoste. Sijui jinsi ya kulifanya ili kwamba kila mtu atafahamu ya kwamba si wazo langu kwamba—kwamba mimi nina—ninawapinga hao ndugu, dada; hilo ni kosa. Mimi ninaeleweka vibaya sana, wala sijui ni kwa nini. Mnaona? Watu wanafikiri mimi siamini katika watu kwenda kanisani. Huo ni uongo mtupu. "Inatupasa kukusanyika pamoja, na zaidi sana tunapoona ile siku ikikaribia." Mnaona? Inatubidi kukusanyika katika umoja. Huenda tusininii . . .

27 Kama niliishi katika mji fulani na hawakuwa na kitu kule ila . . . vema, kanisa fulani (sitaki kutaja jina lo lote), lakini

kanisa lo lote tu, kama waliamini jambo moja tu, ya kwamba Yesu alikuwa ni Mungu, mengine yote si kweli, ningehudhuria kanisa hilo. Kama siwezi kupata mkate mzima, ni—nitakula kipande kimoja. Unaona? Nitaenda nikasikilize, nikamwabudu Bwana, na kumwonyesha ya kwamba ninatekeleza sehemu yangu, ninataka Yeye ajue mimi ni hai. Mimi—mimi ninataka kila mtu ajue niko upande gani. Ninakusanyika pamoja na Wakristo, na huko ninaabudu na—na kumtumikia Bwana.

28 Lakini ni vigumu sana, mimi . . . lilikuwa likinitatiza sana, ndipo nikapata kwamba hata Bwana wetu alifahamika vibaya katika mambo mengi sana. Angesema lo lote, nao wangeninii . . . angefahamika vibaya. Ninakisia inabidi tu kuwa namna hiyo. Lakini wale walio na hekima watafahamu. Unaona? Biblia ilisema jambo hilo. Watalishika.

29 Kwa hiyo asubuhi ya leo wakati nikisema jambo hili . . . Nami nilisema, "Sasa, wao—wao wanaishia jina la Ukristo, bali wanazaa tunda baya. Lina tunda la kimadhehebu. Wanaweka kitu fulani, nao wanaishi kwacho, na kuishi kutokana na ule Uhai."

30 Ni vile nilikuwa nikijaribu kusema jana usiku, roho hiyo inaweza kubatizwa katika Roho huyo na bado asiwe Mkristo. Unaona? Unaishi kutokana na Uhai ule ule, lakini matunda unayozaa yanaonyesha wewe ni nani. Unaona? Hiyo ni kweli. Unaona? Wanaweza kufanya ishara zote, na kuwaombea wagonjwa, na kuponya wagonjwa, na kufungua macho, na kutoa pepo, na—na kufanya mambo haya yote, wakiishi moja kwa moja kutokana na Uhai ulio mle ndani, bali wangali ni mlimau. Unaona? Hiyo ni kweli. "Matunda, unajulikana," Yesu alisema. Na kwa hiyo basi tunaona . . .

31 Na wakati nilipotoka jukwaani, kiongozi huyu mkuu alisimama, akasema, "Humaanishi jambo hilo," akasema, "sote tunajua ya kwamba tumepandikizwa." Vema, hiyo ni kweli kwamba tumepandikizwa, tumepandikizwa kwenye shina, hiyo ni kweli; lakini si kwenye ule Mzabibu, kupandikizwa. Kwa hiyo basi akasema . . . akaanza kwa namna fulani—kwa namna fulani kunikashifu kidogo.

32 Na kulikuwako na kijana mwanamume pale, nafikiri ni wa jamii ya wacheza sinema fulani. Jina Lake ni Danny Henry, naye alikuwa mvulana wa Kibatisti. Vema, alikuja jukwaani akanikumbatia kwa mikono, na kusema, "Ndugu Branham, natumaini jambo hili halisikiki la kukufuru, lakini" kasema "ninaamini hayo karibu yangekuwa ndio sura ya 23 ya Ufunuo."

33 Nami nikasema, "Asante."

34 Ndipo akaanza kusema jambo lingine na kuanza kunena kwa lugha, mvulana Mbatisti. Na wakati alipofanya namna hiyo, kulikuwako na mwa—mwanamke kutoka hapa Louisiana, alikuwa Mfaransa, mwanamke mnene, akaandika fasiri yake.

35 Vema, halafu kulikuwako na jamaa mwingine mdogo ameketi hapa aliyekuwa Mfaransa, akaandika yale aliyosema. Wakalinganisha waliyoandika, na wote wawili walikuwa wako sawa.

36 Ndipo mvulana mkubwa, mwenye nywele nyepesi aliyekuwa amesimama nyuma kabisa, kwenye Mkahawa wa Clifton, akajitokeza. Akasema, "Hebu nione maandishi hayo."

37 Nikaenda kuona yalivyokuwa, na hayo yote matatu yalikuwa na tafsiri ile ile. Alikuwa ni mkalimani wa U.M., mkalimani wa Kifaransa. Na yalisema hivi:

> *Kwa kuwa umechagua njia hii iliyo nyofu na nyembamba, njia iliyo ngumu, umefanya hivyo kwa hiari yako.*
>
> *Lakini ni uamuzi mzuri jinsi gani uliofanya, kwa sababu ni NJIA YANGU.*

Unaona? Na kasema . . . na akaendelea kusema basi:

> *Jambo hili lenyewe ndilo litakalotimiliza, na kufanya na kutimiliza, ule ushindi mkuu sana katika ule Upendo wa Kiungu.*

38 Unaona, daima, hata katika Kifaransa, kitenzi mbele ya kielezi pale katika—katika—katika hiyo fasiri. Kwa hiyo katika hilo nisingeweza kusema . . . Musa, alichagua, ilimbidi kuchagua. Sote tunapaswa kuchagua na tufanye vizuri kabisa tuwezavyo. Na Mungu . . . Mimi ninaheshimu ujumbe wa mtu ye yote ambao ametoa juu ya Mungu. Mimi . . . hata uwe ni nini, ninauheshimu huo kwa moyo wangu wote.

39 Sasa, namwona Ndugu fulani kijana aliyekuja muda kidogo uliopota, Ndugu Stringer, nafikiri anatoka huko Louisiana . . . ama Mississippi, alituletea picha chache hapa ambazo mmetuona tukiziangalia. Ilikuwa ni ya Malaika wa Bwana, wakati alipotokea. Ni wangapi wamesikia hadithi hiyo? Nadhani kila mmoja wenu hapa amesikia. Mmeyapata hayo kwenye kanda, na kadhalika.

40 Sasa, niliambiwa habari hizo asubuhi moja saa nne, nilipokuwa nimesimama chumbani mwangu Indiana. Akaniambia nitakuwa Tucson, itakuwa ni wakati wa asubuhi na mapema, nitakuwa nikiondoa kichomanguo (tunavyoviita hapa, kichomanguo) kutoka kwenye mguu wa suruali yangu. Ndipo Malaika saba wakaja na kulipua hii, ndipo ardhi ikapasuka na kila kitu, kuninii . . . miamba ikabingirika kutoka milimani, na Malaika saba wakasimama pale.

41 Ndipo nikasema, "Vema . . . " Nilimwambia mke wangu, naye yuko mahali fulani hapa asubuhi ya leo, "Tayarisha kila kitu maana hakuna njia mwanadamu angaliweza kustahimili huo," nikasema, "atoke katika huo. Ninaenda Tucson, kazi yangu

imekwisha hapa duniani. Ninaondoka niende nyumbani kuwa pamoja na Bwana Yesu."

42 "Vema," akasema, "una hakika?"

43 Nikasema, "Ndio. Naam, hakuna mtu angaliweza—angaliweza kustahimili huo. Hakuna namna ya kufanya jambo hilo."

44 Ndiyo tu nimalize kuhubiri *Nyakati Saba za Kanisa*. Hapo ndipo nilikuwa nimemwita maskini Ndugu yetu hodari, Jack Moore kumuuliza kuhusu jambo hili, Yesu, katika Ufunuo 1, akisimama pale na nywele nyeupe na kila kitu.

45 Nikasema, "Yeye alikuwa ni kijana Mwanamume." Na hapo ndipo ule ufunuo ulipokuja kwamba hiyo aliyovaa ilikuwa ni wigi, wala si Yeye; Yeye ana wigi (na mimi sikuwaweza kuelewa na jambo hilo), kwamba ni Mungu Mkuu. Na mahakimu wa kale katika Israeli walifanya hivi, walipaswa wavae wigi nyeupe. Na nyeupe inawakilisha usafi. Na mahakimu wa Kiingereza mpaka wakati huu, katika mahakama kuu za Uingereza, huvaa wigi nyeupe wanapotoka, kwa sababu hakuna sheria nyingine inayoshinda yao duniani. Unaona? Nao ni hakimu mkuu.

46 Nami ninakumbuka nilienda kule Arizona na kila kitu, nilikuwa nikijaribu nilivyoweza kuninii…niliogopa sana. Nilienda kwenye mkutano wa Phoenix. Mnakumbuka nilihubiri Ujumbe, *"Mabwana, Ni Wakati Gani?* Mnaukumbuka huo? Nilisema ya kwamba niliona jambo hilo, nikasema, "Kabla halijatukia, kumbukeni, BWANA ASEMA HIVI, 'Jambo fulani litatukia.'" Labda mnazo kanda hizo kwenye maktaba yenu ya kanda sasa. Na humo nilisema, "Mnakumbuka sasa yale maono ambayo hayashindwi hata kidogo. 'Jambo fulani litatukia.' Mnakumbuka!"

47 Na siku chache baada ya jambo hilo, nilikuwa nikishikwa na wasiwasi, ndipo nikawazia, "Ni kitu gani hiki? Je! nitakufa? Kama…Ninatumaini ni kitu cha haraka upesi ili nipate kukipitia. Sitaki kukawia."

48 Ndipo asubuhi moja Bwana akasema, "Panda juu kwenye kilele cha Genge Kuu la Sabino."

49 Nami nilikuwa huko juu nimeinua mikono yangu, nikiomba. Nikasikia kitu fulani kikianguka kwenye mkono wangu. Ilikuwa ni upanga. Sasa, unaweza tu kuwazia vile ungejisikia, mtu ukiwa umesimama pale peke yako na hiki hapa una kisu mkononi mwako kirefu *hivi*. Nikakichomoa na kukiangalia. Kilikuwa ni kisu tu, kimoja cha hivyo…na mimi ninaogopa kisu, hata iweje. Nacho kilikuwa na—kilikuwa na chu—chuma, kitu kama moja ya visu hivi, kama chuma ama cho chote kile, kikali sana na chembamba. Kilikuwa katika ala *hapa* ambapo wale wanaopigana kwa panga walikuwa wakininii, wakijihami wasikatane mikono, na kilikuwa na lulu kwenye mpini wake

hapa. Kilienea mkononi mwangu vizuri sana. Vema, nikasugua uso wangu na kuangalia nyuma.

Mahali papo hapo, hivi majuzi, nikaona maskini hua mdogo akishuka. Nitawaambia juu yake badaye.

50 Basi nilikuwa nimeshika hicho mkononi mwangu, nikawaza, "Ajabu hii. Sasa, Bwana, mimi . . . je! ninaenda wazimu? Hakuna mtu hapa. Niko maili nyingi mbali na binadamu ye yote na huu hapa upanga. Nilikuwa nimeinua mikono yangu juu, basi umetoka wapi?" Kisha nikawaza, "Hiyo ni ajabu kuu. Sasa hebu angalia hapa, ni upanga; unaona, niliugusa, na ulikuwa ni upanga." Ndipo nikasema, "Hakuna mtu hapa anayesimama hapa. Niko kwenye kilele cha miamba hii, moja kwa moja juu kabisa ya mlima." Wala hata usingeweza kuona Tucson kutoka mahali hapo, ilikuwa mbali sana huko chini.

51 Nikawaza, "Sasa, ajabu hii. Sasa, haina budi katika mahali fulani hapa, yuko mtu fulani ambaye anaweza kuumba na kutengeneza upanga na kuuweka mkononi mwangu." Nikasema, "Inaweza tu kuwa ni Mungu yeye yule aliyeumba ndama kwa ajili ya Ibrahimu, angeweza kuumba hao kuchakuro" ambao mmewasikia habari yao. Basi nikasema, "Hivi hapa vitu, vitu vitatu mbalimbali ndani yake, nami ninaushika mkononi mwangu ukiwa halisi tu kama kitu cho chote kile ningaliweza kushika mkononi mwangu."

52 Ndipo nikasikia Sauti, ikasema, "Huo ni ule Upanga wa yule Mfalme!"

53 Basi nikawaza, "Sasa, hiyo imetokea wapi? Ilikuwa moja kwa moja pale kwenye miamba hiyo mahali fulani." Nami nikainua mkono wangu *hivi*, na kusema, "Upanga wa mfalme fulani." Kisha nikaangalia kote kote, na huo upanga ulikuwa hapo tena. Nikasema, "Upanga wa mfalme." Hiyo ni kuninii . . . wao hupandisha mashujaa cheo kwa—kwa upanga, nadhani hiyo ni kweli, jeshi ama kwa njia fulani, wanawapandisha cheo kwa huo. Basi nikasema, "Vema, labda huo ulikuwa wa kazi hiyo. Ina maana kwamba labda nitawekea wahudumu mikono, ama kitu kama hicho, kuwafanya wahudumu." Ndipo ni- . . .

54 Sauti ikanena tena, ikasema, "Upanga wa YULE Mfalme!" Si mfalme *fulani*,Upanga wa YULE Mfalme! Unaona?

55 Nikawaza, "Sasa, aidha mimi ninashikwa na kichaa, akili zangu zimefyatuka, ama kuna jambo fulani linalotukia, kuna mtu fulani amesimama hapa karibu na mimi."

56 Basi ndugu zangu, mambo haya ni kweli. Si—sijui jinsi ya kuwaelezea, daima mmeona jambo hilo likitukia kila mara namna hii. Unaona? Unaona? Ni ninii . . . Sikuweza kuelewa na jambo hilo. Kwa hiyo . . . Ni hisia ya ajabu sana.

57 Mara nikawaza, "Sasa, ye yote huyo aliyenena na mimi maishani mwangu mwote, tangu nilipokuwa mvulana mdogo

sana, amesimama papa hapa, wala siwezi kumwona kabisa." Nikasema, "Ati Upanga wa *yule* Mfalme?" Huo ungekuwa... Mungu ndiye *yule* Mfalme. "Na upanga huu hi nini?"

58 "Neno, limewekwa mkononi mwako." Kasema, "Usiogope kufa, ni huduma yako."

59 Loo, jamani! Nikashuka moja kwa moja kutoka kule mlimani; nikilia, nikipiga makelele, kwa nguvu zangu zote, nikiruka juu ya miamba. Nikateremka huko chini, nikamwambia mke wangu, nikasema, "Sitakufa, unaona, ni—ni—ni huduma yangu tu." (Nilimwambia amwangalie Billy Paul hapa, na awachukue watoto. Nikasema, "Sasa, sina cho chote, lakini kanisa litahakikisha ya kwamba nyote hamkosi chakula na kadhalika, nami nita—nitakutana nawe ng'ambo ya pili.") Na—naye... Nikasema, "La, sitakufa, ni jambo fulani kuhusu huduma yangu."

60 Siku chache baada ya hapo nilikuwa nikitoka mkutanoni; nilipokea telegramu ya kurasa tatu, ilikuwa imetoka Houston, Texas. Na yule mtu aliyenikosoa sana usiku ule Malaika wa Bwana alipopigwa picha, picha Yake ilipopigwa kule Houston, alinipigia simu, akasema... alituma simu, mkewe akasema, "Ninajua, Ndugu Branham, wewe una shughuli nyingi. Mwanangu, mvulana wa dada yake Ted Kipperman, anangojea kunyongwa kwenye kiti." Kasema... (vipi kama huyo angekuwa ni Billy Paul?). Akasema, "Yeye na msichana mmoja mdogo hawana budi kufa." Nanyi nyote mlisoma jambo hilo kwenye gazeti, bila shaka. Kisha akasema, "Tumaini tulilo nalo tu ni wewe uje na kufanya mkutano na kuwakusanya watu pamoja."

61 Naye Raymond Huckstra tayari alikuwa ameniandikia mara nyingi, lakini unajua, nilikuwa nimepanga pale kwenye mkutano huo kwenda safari ya kuwinda pamoja na Bw. Mac Knelly na hao wengine. Basi nikawaza, "Vema, kama nikiwaacha hao watoto wafe na nisitie jitihada zangu, kamwe sitaweza kwenda kuwinda tena."

62 Basi nikasema, "Vema, nitakuja." Nikaenda kule Houston, nikafanya mkutano, na bila shaka ninii... hawakuwaua, walininii tu... waliwaacha huru. Na hivyo ndivyo waivyotaka wafanye, kuwaachilia tu. Kwa hiyo hiyo ni kama miaka ishirini na moja, nadhani, huko—huko Texas.

63 Kwa hiyo basi, na nikirudi, nilipanda kwenda mlimani na niliambatana na Ndugu Fred Sothmann. Yeye yuko hapa mahali fulani. Ndugu Fred, uko wapi? Papa hapa. Ndugu Fred Sothmann, Ndugu Gene Norman; siku moja, tulipokuwa kule siku ya pili, Malaika wa Bwana alishuka moja kwa moja kambini mahali tulipokuwa, na kuanza kunena juu ya watoto wao na mambo yale waliyokuwa wanafanya.

64 Niliondoka nikarudi kilimani. Nami tayari nilikuwa nimempata nguruwe wangu mwitu, na nilikuwa nikijaribu

kumfukuza mmoja kumwelekeza kwa Ndugu Fred. Kwa hiyo niliona mahali walipokuwa wanakula kando ya kilima, ndipo nikasema, "Vema, sasa, nitakwambia la kufanya, Ndugu Fred." Nikasema, "Sasa, wewe uende mahali pale asubuhi." Tunaenda kule mchana, tupande mlima. "Basi uende kule mchana, mimi nitaenda upande wa pili. Sasa, sitampiga ye yote risasi, lakini kama wakikimbia upande huu, nitarusha risasi mbele yao na kuwarudisha. Basi chagua aliye mkubwa."

65 "Vema," akasema.

66 Kwa hiyo Ndugu Fred akaenda kule. Na Ndugu Gene Norman (sidhani Ndugu Gene amekuja, sivyo?), alikuwa—alikuwa ng'ambo ya pili. Wengi wenu mnafahamu Gene Norman, rafiki msiri wa wengi, ndugu mzuri. Naye alishuka chini kidogo. Ambako, hao nguruwe, hawakuwako tu asubuhi hiyo. Nami niliweza kumwona Ndugu Fred, nikampungia mkono, alikuwa kama maili moja kutoka kwangu. Vema, nikawaza, "Hivi inawezekana walienda wapi?" Nikaingia kwenye korongo kubwa, kisha nikashuka, nikawaza, "Nitaona kama ninaweza kupata waliko." Nikaanza kurudi. Ilikuwa ni baadhi tu ya mapambazuko, jua ndio kwanza lianze kutokeza.

67 Basi nikazunguka genge kubwa mno, loo, jamani, mamia na mamia ya futi, miamba mikubwa tu katika lile genge kuu kule, hizo kuta kubwa. Na ilikuwa kwa namna fulani inakuwa . . . jua lilikuwa linachomoza, kama saa moja, nadhani, ama kitu kama hicho. Basi nikaketi na nilikuwa nikiangalia huku na huko, ikatokea ya kwamba niliangalia kwenye mguu wa suruali yangu na hiyo hapo kishomanguo, mbegu yenye manyoya, manyoyanyoya. Ndipo nikasema, "Unajua, hiyo inaonekana ni ajabu. Unajua, Malaika wa Bwana aliniambia ningekuwa kama maili arobaini kaskazini-mashariki mwa Tucson, nitakuwa nikiondoa mbegu ya kishomanguo kutoka kwenye mguu wa suruali yangu." Mnakumbuka jambo hilo? Mnaona? Naam, bwana. Mnaona? Nikasema, "Ajabu hiyo." Nilikuwa nimeshika mbegu hiyo.

68 Na mara nilipoangalia juu tu, niliona nguruwe kama ishirini hivi wakiwa kama fiti mia tano kutoka kwangu, wakatoka wakila majani haya ya faila kisha wakalala. Nikasema, "Sasa, laiti ningalimpata Ndugu Fred nimpeleke mahali pale, atampata nguruwe wake pale pale. Lakini ninajua yuko maili moja ama mbili kutoka kwangu sasa. Kwa hiyo," nikasema, "kama ningeweza kuvuka kilele cha kilma hiki bila wao kuniona, nipande juu kupitia kwenye mreteni huu pale," nikasema, "kama nikizunguka upande huu, kuna mkondo wa kulungu unaoshukia upande huu, ninaweza kukimbia kule na kutoweka njiani. Kisha nitundike kipande kidogo cha karatasi hapa ambapo ninajua nitaendea kidole gani, kwenye genge hili, na kumpata Ndugu Fred kule kwa wakati mzuri."

69 Nilitupa chini mbegu hii ya kishomanguo, nikasahau jambo Hilo. Ndipo nikaanza kutelemka kuvuka kilima kwa urahisi sana kisha nikaangalia nyuma, hawakuniona, basi nikateremka mbio nikafikia kwenye mkondo huu wa kulungu. Nilikuwa nimevaa kofia kubwa pana nyeusi. Nikaanza kukimbia mbio sana kupitia kwenye magenge haya, ndipo likatukia.

70 Ardhi nzima ikatetemeka, kila mahali. Miamba ukubwa *huo* ikafingirika chini, mavumbi yakiruka namna *hiyo*. Ndipo nikaangalia, na mbele yangu walisimama Malaika saba; vile vile tu ilivyokuwa. Nilijisikia kama nilikuwa nimesimama juu mbali sana kutoka ardhini. Kwanza, nilifikiri mtu alikuwa amenipiga risasi, wajua, nikiwa nimevaa hiyo kofia nyeusi; ilionekana kama ngiri, hata hivyo, unajua wao ni weusi. Nilifikiri mtu fulani alikuwa amenipiga risasi, kama. . . akiwa karibu sana. Ndipo ni—nikaona basi ilikuwa ni nini. Vema, mara tu. . . nikapata agizo langu, na Maandiko, "Mihuri Saba ambayo ni zile siri saba." Unaona?

71 Mtu fulani akaniambia, akasema, "Sasa. . . " Loo, akasema, "Vema, sasa, siku moja Bwana labda (wewe kwa kuona maono, Ndugu Branham) atakufunulia mambo haya ni nini, sote tunaweza kuwa karibu na Mungu na tuwe na nguvu zaidi kuliko tunavyopata katika kunena kwa lugha na kadhalika."

72 Nikasema, "Haiwezi kuwa namna hiyo."

73 Maana, unaona, ninaamini Neno kwamba ni Kweli. Na Biblia ilisema, "Ye yote atakayeongeza neno moja ama kuondoa Neno moja Kwake." Lazima iwe katika Neno hili. Unaona? Ni zile siri ambazo watu hawakuziona. Vema, papo hapo ndipo palitokea Ujumbe wangu wa *Uzao wa Nyok*a na Imani ya kweli ya usalama wa mwamini.

74 Mimi siwadharau ndugu zangu wa Kipresbiteri hapo, na ndugu fulani wa Kibatisti jinsi mlivyo na usalama. Sisemi jambo hili kusudi niwe tofauti, lakini hamkulipata jambo hilo sawa. Unaona? Hiyo ni kweli. Unaona? Lakini, nilikuwa nimekosea, pia. Lakini wakati Malaika anaposimama kutoka Mbinguni na kukwambia, na hili hapa katika Maandiko, Hiyo ni kweli. Unaona? Hiyo ni kweli. Unaona, Yeye daima hunena sawasawa na Maandiko.

75 Ndani humo niliangalia mpaka hiyo duara ikapaa juu, ikaanza kwenda juu, nao wakabadilika kuwa nuru ya kisiri, kama ukungu. Jinsi kabisa vile. . . Ni wangapi waliona picha yake iliyopigwa huko Huston? Mnakumbuka jambo hilo? Mnaona? Vema, Hivyo ndivyo hasa hii ilivyokuwa. Iligeuka ikawa jambo lile lile, ilizidi kwenda juu zaidi na zaidi.

76 Nilikuwa ninakimbia na kukimbia, nikijaribu kumpata Ndugu Fred na hao wengine. Baada ya kitambo kidogo, kama nusu saa baadaye, niliweza kumwona huko chini kabisa, akipunga mikono yake; na Ndugu Gene akija, akipunga mikono.

Walijua jambo fulani lilikuwa limetukia. Na kwa hiyo basi nikawafikia. Huyo ni Ndugu Fred anayeketi papo *hapo*.

77 Wakati ilipokuwa ikienda juu, sikujua ya kwamba vituo vya uchunguzi na kadhalika, mpaka kufikia Mexico, vilikuwa vikipiga picha hiyo. Gazeti la *Life* lilichapisha picha Yake lilipokuwa likipaa juu. Na wengi wenu . . . Hili hapa gazeti la Life limechapisha picha Yake. Kitu kisichofahamika hapa, nao walisema hawajui kilikotoka; kiko juu sana. Kiko juu ya maeneo yote ya anga na cho chote kile . . . Kiko juu sana hakiwezi kuwa ni ukungu, kwa sababu kitu hicho kiko maili thelathini kwenda juu na maili ishiri na saba kutoka upande mmoja mpaka mwingine baada ya kwenda juu kiasi hicho. Hakuna hata unyevu wala cho chote kule juu, unaona.

78 Nao waliwazia kuhusu ndege; kwa hiyo wakachunguza mahali pote, hakuna ndege zilizoruka juu siku hiyo. Unaona, imewalazimu kuchunguza, kwa sababu ya kutikiswa kwa madirisha na kadhalika. "Hakuna ndege kule juu." Hili hapa moja kwa moja gazetini, litakwambia jambo lile lile. Basi—basi likazidi kusonga mbele. Na leo moja kwa moja katika . . .

79 Hili hapa katika gazeti la *Sayansi,* ambapo, hawawezi kufahamu jambo hilo, hawajui Hilo ni nini.

80 Huko Tucson, chuo kikuu, rafiki yangu mmoja alienda kule hivi majuzi naye alikuwa akizungumza nao kuhusu ya jambo hilo. Kasema, "Hatuwezi kuelewa ni kitu gani . . . "

81 Nikasema, "Usiseme lo lote, halitafaa kitu. 'Usitupe lulu zako mbele ya nguruwe.'" Unaona? Ni kwa ajili ya Kanisa, kwa Wateule, walioitwa watoke. Unaona?

82 Na halafu kila mmoja alikuwa anakuja, akisema, "Ndugu Branham, ninaona picha yako hapa. Ninaona hii. Mimi . . . " Unajua jinsi ilivyo. Lakini huo—huo mtandao mrefu kama huu alio nao huyu ndugu hapa ambapo . . . Samahani [Ndugu Branham anachukua hiyo picha—Mh.]. Hivi ndivyo lilivyoanza kupaa juu, likielekea juu. Kwa kweli *hili* lilikuwa kwenye mkono wa kulia. Nanyi nyote mnakumbuka nilisema, "Yule Malaika maarufu alikuwa ndiye aliyenena na mimi, alikuwa mkono wa kulia," hata kabla halijatukia. Mnakumbuka? Mbawa Zake zilielekea nyuma namna *hiyo*. Hizo hasa ni mbawa za Malaika huyo alipopaa. Unaona, alipo . . . Kwa hiyo wakaanza kupiga picha kwa sababu lilikuwa ni la kisiri sana. Lakini wakati picha ya mwisho, wakati ilipojiumba Yenyewe ndani ya mbingu na kadhalika, ndio hii hapa kama vile *Look* hapa lililivyoichukua. Unaona jinsi lilivyopaa juu walipoanza tu kuliona, unaona. Ndipo hapo ikaja ninii—ile picha yenyewe halisi na ya mwisho, wakati lilipoumbika.

83 Hawajui mahali lilipotoka au mahali lilipoenda, wangali hawajui. Sayansi imeduwazwa kabisa juu yake, haijui kile kilichotukia. Lakini tunajua; "kutakuwako na ishara juu

mbinguni." Tunajua hilo. Unaona? Naye aliahidi mambo haya. Unaona? Na sababu tu ya hii kuruhusiwa kupigwa . . .

84 Lakini ninajua sisi ni watu tu wa nyumbani hapa asubuhi ya leo. Kama niliwahi kujifanya mjuvi kwenu ndugu ama kwenu dada, naomba mnisamehe. Sikusudii kuwa hivyo. Ninasimama . . . nimeketi hapa asubuhi ya leo nikizungumza mbele ya watu ambao ni wasomi, watu wenye bongo; mimi si— sina elimu, hata siwezi kutamka Maandiko yangu vizuri. Nina mlango mmoja wa kusoma asubuhi ya leo, mimi . . . nilikuwa nimwombe mmoja wa ndugu hapa anisomee mlango huo, maana hata siwezi kutamka majina yaliyo katika mlango huo, I Mambo ya Nyakati 13, (kama ukipenda, Ndugu Jack, unaweza kuutafuta), kwa ajili ya somo langu. Hata si—siwezi kutamka majina hayo, nitamwachia asome, maana yeye anaweza kuyatamka.

85 Nami ninajua ninazungumza na watu wenye bongo. Lakini, ndugu, mambo haya yanafanyika kusudi msiangalie kutokujua kusoma kwangu, bali mwamini ninawaambia Kweli. Ni Mungu akiwaambia Kweli. Hiyo ni Kweli. Unaona?

86 Sasa, na wakati ninapozungumza juu ya madhehebu, sikusudii mwe wakatili sana na . . . La, simaanishi msiende kanisani kwenu. Nendeni kanisani kwenu, yale mnayopaswa kufanya. Bali msijiunge na hayo madhehebu, kwa sababu siku moja nitawaambia na kuwathibitishia kwa Maandiko, ni alama ya mnyama. Nanyi kumbukeni tu, ni alama.

87 Ninahubiri . . . Singehubiri jambo hilo kwenye kanisa la Ndugu Jack, yeye angeniambia, "Endelea na kuhubiri"; lakini ninaenda Maskanini, utachukua kama masaa manne. Na somo langu ni: "*yule mnyama hapo mwanzo na mnyama hapo mwisho, kupitia mkondo wa nyoka*." Unaona? Utachukua kama masaa manne. Nimeandika Maandiko yangu yote. Yule mnyama tangu mwanzo, alikuwa mnyama katika Bustani ya Edeni, yeye ni mnyama hapo mwisho, na nionyeshe ya kwamba yeye ni mtu wa dini na ni madhehebu (aliyeunda madhehebu); na akaja moja kwa moja kupitia kwenye mkondo wake, na niwathibitishie kwa Maandiko ya kwamba ndivyo alivyo. Sikujua jambo hilo mpaka Roho Mtakatifu aliponipa somo hilo hivi majuzi kule juu.

88 Sasa, katika jambo hili, nilikuwa nikiangalia jambo hili siku moja, nikisimama, na kitu fulani kikaniambia . . . nikikiangalia, nami nikafikiria . . . Ndugu Hickerson, mmoja wa wadhamini wangu . . . ama mashemasi katika kanisa la Jeffersonville . . . Kama mimi siamini kwenda kanisani, basi kwa nini niwe na makanisa? Tulikuwa nayo kila mahali nchini, yameunganishwa hivi majuzi usiku, kila maili mia mbili mraba kulikuwapo na kanisa langu.

89 Sasa, picha hii—hii, nilikuwa nimesimama, nikiiangalia, na kitu fulani . . . nilikuwa nimesimama chumbani mwangu. Kitu fulani kikasema, "Igeuze upande wa kulia." Nikasikiliza.

90 Ninajua jambo hilo linasikika kama kwamba mtu fulani ameharibikiwa na akili kidogo, lakini, unaona, kama nilivyosema hivi majuzi usiku, mambo haya yote makubwa ni ya kielimu sana . . . Sasa, mimi sipingi jambo hilo. Kumbukeni, hatuna budi kuwa ninii . . . Pelekeni watoto wenu shuleni wapate elimu na kadhalika, lakini nitawaambia papa hapa sasa hivi, haitawasaidia hata kidogo katika ulimwengu ujao, kwa maana kutakuwako na ustaarabu mwingine. Yote haya . . . mbali sana na huu. Ustaarabu huo hata hautakuwa na ninii yo yote . . . hautakuwa na shule zo zote, hautakuwa na kifo, hakutakuwako na dhambi yo yote. Huu una hayo yote; haidhuru tustaarabike namna gani, kifo kinazidi kuongezeka wakati wote. Unaona? Huo hautakuwa na mauti. Lakini sasa hivi hatuna budi kuwa na shule, hatuna budi kuvaa nguo, ha- . . .

91 Nilikuwa nizungumze asubuhi ya leo juu ya *Edeni ya Shetani* (wengi wenu mna kanda yake), *Edeni ya Shetani*. Yeye amefanya bustani nyingine ya Edeni, imemchukua miaka elfu sita kuifanya, kama tu Mungu alivyoifanya Yake hapo mwanzo. Mungu alifanya Edeni Yake, na Shetani akaiharibu. Sasa Shetani amefanya Edeni yake mwenyewe, na Mungu ataiangamiza (hiyo ni kweli) na kuweka Yake mwenyewe.

Kitu fulani kikaniambia, "Igeuze mkono wa kuume."

Nikawaza, "Nafikiri ninaiangalia vizuri."

Kasema, "Igeuze *kuume*."

92 Nikawazia, "Labda sauti hiyo inamaanisha niigeuze *kwenye* upande wa kuume." Na nilipofanya jambo hilo, unaona ni kitu gani: *Kichwa cha Kristo* kilichochorwa na Hoffman, akiwa na umri wa miaka thelathini na mitatu. Hapa, angalia hapa ndani, angalia ndevu Zake nyeusi, uso Wake, macho Yake, pua Yake, na cho chote kile. Angalia sehemu ya nywele Zake hapa zikitokeza. Na ametiwa wigi kwa wigi nyeupe ya Malaika kuonyesha ya kwamba Ujumbe wa Yeye kwamba ni Mungu ni Kweli. Yeye ni Hakimu Mkuu wa ulimwengu, Hakimu Mkuu wa Mbingu na nchi. Yeye ni Mungu, na si kitu cho chote kingine ila ni Mungu. Yeye ni Mungu aliyedhihirishwa katika umbo la kibinadamu linaloitwa Mwana wa Mungu, ambapo Mwana alikuwa ni kinyago. Na kama hilo haliufanyi Ujumbe wetu kweli kabisa: umetambulishwa na Maandiko, umetambulishwa katika huduma, umetambulishwa kwa Uwepo Wake, yeye yule jana, leo, na hata milele. Kwa hiyo hiyo Mihuri Saba ni Kweli, ndugu. Huenda msikubaliane nayo, lakini ketini chini tu na msome kwa moyo mkunjufu wakati mmoja, acheni tu Roho Mtakatifu awaongoze kutoka . . .

93 Hapa, wakati Ndugu Jack . . . nilimpigia simu kabla sijaanza kuhubiri huu na nikazungumza naye wakati mmoja juu ya "Wigi hii nyeupe ilikuwa ni nini?"

94 Akasema, "Vema, Ndugu Branham, ninatangaza ya kwamba ilikuwa katika . . . ilikuwa ni baada ya kufufuka Kwake katika mwili Wake uliotukuzwa." Nilikuwa nikizungumza na Ndugu Jack. Na kuna . . . Sijui juu ya mtu ye yote ulimwenguni ninayeweza kutegemea mafundisho yao juu ya theolojia na kadhalika zaidi kuliko ninavyotaka kumtegemea Ndugu Jack Moore na Ndugu Vayle, na mtu kama—kama hao, wanatheolojia halisi walisoma vitabu vya kila namna na mitazamo mbalimbali kutoka kila kiti. Vema, lakini, unaona, hata na jambo hilo, na rafiki wangu msiri, ni—ni—nisingeweza kulipokea, kulikuwako na kitu fulani ambacho hakingeweza kulipokea.

95 Na basi wakati ilipokuja, hii, ndipo nikaona ni kitu gani. Hizi hapa ndevu Zake nyeusi. Mnaziona, nadhani. Mnaona? Ndevu Zake nyeusi na nywele nyeusi, macho Yake, pua, kila kitu, vizuri sana, na hata sehemu katika nywele Zake inayokuja upande huu. Yeye ni Mungu! Mnaona? Naye yeye yule jana, leo, na hata milele. Na hili ni gazeti la *Look* . . . ama gazeti la *Life*. Nafikiri hii ni . . . Ninasahau ni nakala gani sasa; loo, tarehe kumi na saba Mei, 1963. Hapo ndipo lilipotolewa, kama mtu ye yote anataka gazeti hilo. Ni picha ile ile iliyo na Rockereller na na nanii wake—mke wake upande wake wa nyuma. Na hili ni gazeti jipya la *Sayansi* hii ni kwamba "bado lingali ni jambo la kisiri."

96 Kwa nini nikasema mambo haya? Ili yawape mwelekeo mdogo wa mambo tunayojaribu kusema, ambayo Mungu anayatambulisha mbinguni na nchini kwamba ni kweli, huu utambuzi, maono. Tuna kuigiza kweingi sana, sikuzote tunako. Lakini kumbukeni, kabla hapajakuwepo na dola ya bandia, hapana budi kuweko na dola ya kweli; kwanza hapana budi kuweko na dolla ya kweli, halafu zinatolewa kutoka kwa hiyo. Ni kama tu vile tulivyokuwa na Musa halisi na Haruni halisi, ndipo tukawa na Yambre na Yane baada ya wao. Unaona vile yote yanavyotokea? Wanaliona kisha wanajaribu kuiga hilo, wakati kweli kuna *moja* iliyo ya asili. Hiyo ni kweli. Sisemi jambo hilo kuumiza mtu au kumvunjia mtu heshima, ama kuweka jambo lo lote vibaya, bali ni kwa ajili ya Kweli tu; mpate kujua ya kwamba mimi . . .

97 Ninakuwa mzee, na ninajua wakati wangu si mrefu sana. Yesu akikawia, huenda nikaninii . . . ningeweza kuishi kitambo kidogo; lakini ninajua siku moja moyo huu utapiga pigo lake la mwisho, na mimi ninaingia katika chumba kikubwa, chenye giza pale kinachoitwa mauti. Lakini wakati hilo litakapokuja, sitaki kitu cha kunilazimu niangalie nyuma, kujaribu kukitubia. Ninataka, nitakapofikia wakati huo, niwe msafi na mtakatifu kwa neema ya Mungu. Ninataka kujifunika katika majoho ya haki Yake, nitakapoingia mle, nikiwa na jambo hili moja moyoni

mwangu: ninamjua katika nguvu za kufufuka Kwake; na wakati atakapoita, nitatoka katika wafu na kuishi pamoja Naye milele. Na ni kusudi langu hapa sasa kujaribu kumfanya kila mtu . . . si kubadilisha theolojia zenu wala cho chote kile, bali kuongeza imani yenu katika ahadi ya Mungu ya siku hii.

Na tuombe:

98 Mungu mpenzi, sisi ni watu wenye shukrani asubuhi ya leo, lakini hata hivyo, Bwana, tunaishi katika ulimwengu wenye giza ambao . . . Hakuna hata mmoja wetu hapa asubuhi ya leo, Baba, ila anayejisikia ya kwamba tu—tunataka kutembea karibu zaidi na Wewe, tunataka mguso huo—huo Wako katika maisha yetu unaoweza kutufanya wapole na kutufanya wenye kupindika ili kwamba uweze kutubadilisha wakati wo wote, utufinyange tuwe wana na binti za Mungu. Hilo—hilo ndilo kusudi letu hapa, Baba, hilo—hilo ndilo lengo langu tu nililo nalo ni kujaribu ku—kuishi mbele Zako na kupata Neno Lako na kulinena kwa wanaume na wanawake ambao . . . si kwamba niwe mtu tofauti lakini ni kujaribu kumheshimu Yeye ambaye amenipa Uzima. Tujalie hayo, Bwana.

99 Jalia asiwepo mtu hapa leo . . . Ama—ama kama . . . Tumeunganishwa asubuhi ya leo, kote nchini, tena. Jalia asiwepo mtu aliye kwenye eneo la sauti yetu atakayelazimika kuingia katika kile chumba kikuu bila kukujua Wewe katika nguvu za kufufuka Kwako. Kama kuna wenye dhambi mahali fulani nchini kote, ambao . . . ama katika jengo hili, jumba hili kuu la mikutano, anayeketi hapa asubuhi ya leo. Kama kuna wale wasiokujua Wewe, jalia hii iwe ndiyo siku ambayo dhamira zao zitatikiswa, zitaamshwa, nao watatambua ya kwamba hawajui ni dakika gani twaweza kuitwa ama tuitwe tukawajibike kwa ajili ya maisha yetu, huko Juu. Na kama jina letu lingali liko kwenye kitabu hicho cha ubua, tutaangamia; lakini kama liko kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, ule Uhai halisi, basi tumeokoka.

100 Na jalia, Bwana, wakati Uhai huo ukisafiri kutoka katika jani na kuingia kwenye chavua, hadi kwenye kapi, halafu kwenye chembe, wakati wakipita asubuhi ya leo kama kuna Uhai fulani unaoingia kwenye chembe iliyo kule nyuma katika huo ubua, utoe leo, Bwana, naomba huo ufuate kusogea kwa ile chembe, kwa kuwa tunaomba hilo katika Jina la Yesu. Amina.

101 Samahani kwa kuchukua muda mwingi sana. Nilisahau hata kwamba haya yalikuwa yako kwenye kipindi cha kule nje, kipindi cha simu.

102 Sasa hebu na tufungue kwa ajili ya somo letu. Na Ndugu Jack, una Biblia yako hapo? Ninapotafuta Maandiko yangu, nitamwomba Ndugu Jack asome Maandiko haya kwa sababu siwezi kutamka majina haya vizuri. Vema, katika Mambo ya

Nyakati 13. . .?. . .[Ndugu Jack Moore anasoma I Mambo ya Nyakati, mlango wa 13—Mh.]:

*Kisha Daudi akafanya shauri na maakida wa maelfu, na maakida wa mamia, naam, na kila kiongozi.*

*Daudi akawaambia jamii yote ya Israeli, Likiwa jema kwenu, tena likiwa limetoka kwa BWANA, Mungu wetu, na tutume watu huku na huku mahali pote kwa ndugu zetu waliosalia katika nchi yote ya Israeli, ambao pamoja nao makuhani na Walawi wamo ndani ya miji yao yenye viunga, ili wakusanyike kwetu:*

*Nasi tujirudishie tena sanduku la Mungu wetu; maana ha—hatukuuliza neno kwa hilo katika siku za Sauli.*

*Nao jamii nzima wakasema ya kwamba watafanya hivyo; kwa kuwa neno hilo lilikuwa jema machoni pa watu wote.*

*Basi Daudi akawakusanya Israeli wote, toka Shihori, kijito cha Misri, hata pa kuingilia Hamathi, ili kwamba walilete sanduku la Mungu kutoka Kiriath-yearimu.*

*Basi Daudi akapanda, yeye na Israeli wote, mpaka Baala, ndio Kiriath-yearimu, ulio wa Yuda, ili kulileta toka huko sanduku la Mungu, BWANA akaaye kati ya makerubi, lililoitwa kwa Jina lake.*

*Wakalipandisha sanduku la Mungu juu ya gari jipya kutoka nyumba ya Abinadabu; na Uza na Ahio waka—wakaliendesha lile gari.*

*Wakacheza Daudi na Israeli wote, mbele za Mungu, kwa nguvu zao zote; na kwa nyimbo, na kwa vinubi, na kwa vinanda, na kwa matari, na kwa matoazi, na kwa tarumbeta.*

*Hata walipofika penye uga wa Nakoni, Uza akaunyosha mkono wake alishike sanduku; kwa maana wale ng'ombe walikunguwaa.*

*Ndipo hasira ya BWANA ikawa juu ya Uza, naye akampiga kwa sababu alilinyoshea sanduku mkono wake, hata akafa pale pale mbele za* Bwana.

*Naye Daudi akaona uchungu, kwa kuwa BWANA amemfurikia Uza: akapaita mahali pale Peres-uza hata leo.*

*Naye Daudi akamwogopa Mungu siku ile, akasema, Nitajileteaje sanduku la Mungu nyumbani kwangu?*

*Basi Daudi hakujichukulia sanduku nyumbani mjini mwa Daudi, ila akalihamisha kando na kulitia nyumbani kwa Obed-edomu Mgiti.*

*Sanduku la Mungu likakaa na jamaa ya Obed— Obed-edomu, nyumbani mwake, muda wa miezi mitatu. Naye*

*BWANA akaibariki nyumba ya Obed-edomu, na yote aliyokuwa nayo.*

103 Asante, Ndugu Moore, kwa kunisomea Maandiko. Sasa, samahani mimi nisingeweza kusoma hayo mimi mwenyewe, lakini si—singeweza kufanya hivyo.

104 Sasa nataka mfungue pamoja nami katika Mariko 7:7, nasi tutasoma vifungu saba vya kwanza vya Marko Mt. mlango wa 7.

*Kisha Mafarisayo, na baadhi ya waandishi waliotoka Yerusalemu, wakakusanyika mbele yake.*

*Nao walipoona wengine katika wanafunzi wake wakila vyakula kwa mikono najisi, yaani, isiyonawiwa, wakalalamika.*

*Kwa maana Mafarisayo na Wayahudi wote wasiponawa mikono*. . . mara nyingi, *hawali, waki—wakishika mapokeo ya wazee wao;*

*Tena* wakija kutoka *sokoni,* hawakutawadha, *hawali. Na yako mambo mengine* yalikuwa— yalikuwa . . . *waliyopokea* kuninii . . . *kuyashika, . . . kuosha vikombe, na midumu, na vyombo vya shaba, na vya mezani.*

*Basi wale Mafarisayo na waandishi wakamwuliza, Mbona wanafunzi wako hawaendi kwa kuyafuata mapokeo ya wazee, bali hula chakula kwa* mkono *najisi?*

*Akajibu akawaambia, Isaya alitabiri vema juu yenu ninyi wanafiki, kama ilivyoandikwa, Watu hawa huniheshimu kwa midomo ila mioyo yao iko mbali nami;*

*Nao waniabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu.*

Na tuombe:

105 Mungu mpendwa, litukuze Neno Lako sasa, na jalia litimize yale liliyokusudiwa. Tutumie kama vyombo kulinena, na maskio yetu kulisikia kutoka Kwako, na mioyo yetu kulipokea. Tunaomba katika Jina la Yesu, kwa utukufu wa Mungu. Amina.

106 Sasa, somo langu kwa muda mfupi ni hili . . . Mimi . . .

107 Tuko tumeunganishwa asubuhi ya leo kwa simu nchini kote. Nami nasikia ya kwamba rafiki yangu mzuri, Roy Borders, anasikiliza, amehangaika sana kuhusu jana usiku. Nilikuwa nimesahau tulikuwa kwenye redio . . . ama kuunganishwa huku jana usiku. Roy, po pote ulipo, iwapo uko San Jose huko kanisani, ama huko kwa kanisa la Ndugu McHughes, ama po pote ulipo, usiogope, ndugu yangu, kila kitu kitakuwa shwari. Tulia, wewe ninii tu . . . Yeye atakujulisha jambo hilo, Roy; usiwe na wasiwasi, mwanangu, mwamini Mungu.

108 Somo langu asubuhi ya leo ni: *Kujaribu Kumtumikia Mungu Bila ya Kuwa Ni Mapenzi ya Mungu*. Sasa, hilo ni somo la

ajabu, na ninatumaini ya kwamba Bwana atatufunulia hili sasa. Kumbukeni: *Kujaribu Kumtumikia Mungu Bila ya Kuwa Ni Mapenzi ya Mungu.* Sasa, hilo laonekana kwamba ni somo la ajabu, nami nitumaini ya kwamba Bwana atufunulia hili sasa. Kumbukeni: Kujaribu kumtumikia Mungu bila ya kuwa ni mapenzi ya Mungu. Sasa hilo linaonekana la ajabu sana. Lakini, katika jambo hili, pengine Mungu anaweza kutusaidia.

109 Jambo jingine ningetaka kusema asubuhi ya leo, ni kwamba tuna furaha kuwa na rafiki yangu miongoni mwetu, rafiki mpenzi wangu, jamaa mdogo. Wengi wenu ninyi watu kwenye redio sasa mnaweza...ama ninii...kwenye mawasiliano ya simu, mnajua huyu ni nani. Leo ni siku yake ya kuzaliwa, ana umri wa miaka tisini na mitatu, Ndugu Bill Dauch anayeketi hapa mbele yangu, mwenye umri wa miaka tisini na mitatu.

110 Miaka kadhaa iliyopita daktari alisema, "Hawezi kuishi." (Ndio kwanza nimwone ameketi hapa sasa.) Chini ya kihema cha oksijeni, na mpenzi mke wake alinipigia simu na kusema, "Ndugu Branham, kama unatarajia kumwona maskini rafiki yako, Bill, akiwa hai, afadhali uje mara moja."

111 Nami...Moja ya tairi zangu ilikuwa imekatwa upande mmoja, gurudumu langu lilikuwa limepasuka, nami nikararua tairi la gari langu nikijitahidi kwenda kumwahi. Nilikuwa ndiyo kwanza ninakuja kutoka kwenye ki—ki— kituo, kituo cha petroli, na ninatoka msalani ambapo nilikuwa nimesimama huko Ohio nikikazana kumwahi, na nilipokuwa nikitoka nikaona ono. Na hapo alisimama Ndugu Dauch, amesimama kanisani huku ametoa mkono wake; likabadilika, ndipo nikakuona ukishuka kuja barabarani na kunipa mkono. Kasema, "Nenda ukamwambie, BWANA ASEMA HIVI.'"

112 Alikuwa na umri wa miaka tisini wakati huo. Alikuwa na mshtuko wa moyo pamoja na moyo kuziba, na kusita kabisa kwa moyo. Daktari hodari sana. Mtu huyo si...hataki...La, sitasema jambo hilo. Yeye ni mtu tu ambaye ana uwezo... kumpata dakatari ye yote anayetaka. Alikuwa na daktari hodari sana wa Kiyahudi aliyekutana nami sebuleni na kusema, "Hakuna uwezekano wa yeye kuishi kabisa."

113 Basi nikaingia ndani na kupenyeza mkono wangu chini ya kile kihema cha oksijeni, nikasema, "Bill, unaweza kunisikia?" Akatikisa kichwa chake. Nikasema, "BWANA ASEMA HIVI, 'sasa hutakufa."

114 Juma moja baada ya hapo, nilipoenda mimbarani kuhubiri Ujumbe wangu, huyu hapa Ndugu Dauch anakuja akitembea ndani kupitia jengo. Na nilipoenda kwenye Mkahawa wa Furr, upande wa pili...ninamaanisha Blue Boar, kwenda huko Louisville, huyu hapa akitoka kwenye gari, akishuka barabarani, ametoa mkono wake; sawasawa na Neno la Bwana. Na hiyo ni miaka mitatu ama minne iliyopita; naye huyu hapa

ameketi hapa kutoka Shreveport ya mbali (anavuka nchi, si kwa ndege sasa, kwa gari) a-ha, ameketi hapa asubuhi ya leo. "Nakutakia siku yenye furaha ya kuzaliwa kwako, Ndugu Dauch." Hiyo ni kote nchini, kutoka kila mahali. "Mungu akubariki!"

115 Nilimbatiza, baada ya kuwa wa utatu, nilimbatiza wakati aliponinii. . .ilikuwa mmoja wa mikutano yangu ya kwanza, wakati ilipombidi Ndugu Banks Wood kumpatia nguo zake (yeye ni mtu mkubwa, kama mnavyoona), ndipo akaingia katika kidimbwi nami nikambatiza akiwa na kama miaka themanini na mitano ama tisini, katika Jina la Bwana Yesu. Alisema hangeweza kujisikia sawa hata kidogo mpaka alipopata usalama huo wa jambo fulani. Ndipo akapata siku ya kuzaliwa ambapo hatazeeka kamwe. Hiyo ni kweli, Nchi ile iliyo kuu. Hata anatarajia kuishi aone kuja kwa Bwana; inawezekana. Lakini kama akilala, yeye. . .nasi tu hai wakati huo, yeye atakuja kwanza. Kweli. Kwa hiyo, Ndugu Dauch, hakuna njia sasa ya kukosa jambo hilo. Wewe uko kwenye njia sahihi. Dumu hapo, ndugu yangu, na Mungu akubariki. Nami ninamshukuru Bwana kwa ajili ya mtu mzuri kama huyo, na kwa kumpa miaka hii yote.

116 Katika Kitabu cha Mambo ya Nyakati, "Kujitahidi kumtumikia Mungu bila ya kuwa ni Mapenzi Yake." Mungu ni mwenyezi, kwanza, tunataka tulielewe. Watu siku hizi hawajui ni kwa nini hatuwezi kuwa na ufufuo. Je! unaamini Mungu ni mwenyezi? Unaona, Biblia inasema hivi.

117 Nasi tunajaribu. . .Kama nilivyokuwa nikizungumza na kundi la ndugu zangu wazuri, ndugu wa Kibatisti, si muda mrefu uliopita, nao walisema, "Ndugu Branham, tunaweza tu kuwa na ufufuo wakati tukichukua Neno, neno kwa neno, ukurasa kwa ukurasa, herufi kwa herufi."

118 Ndipo nikasema, "Ninaamini pia, ukurasa kwa ukurasa." Akasema. . .Nikasema, "Wamekuwa wakijaribu kufanya jambo hilo wakati wote."

119 Akasema, "Lakini hatuna budi kupata tafsiri ya Kiyunani ya Neno, vile inavyonenwa katika Kiyunani.'"

120 Nikasema, "Mimi sikusoma sana, lakini katika kusoma kwangu historia ya kanisa, na Baraza la Nikea, na waazilishi wa Nikea, na kadhalika, walikuwa wakibishana *kule* juu ya Kiyunani. Hiyo ni miaka elfu mbili iliyopita. Mmoja alisema, 'Linamaanisha *hivi*,' na mmoja anasema, 'Linamaanisha *vile*. Neno hilo la Kiyunani linamaanisha hivi.'"

121 Ni kama tu lugha yetu; neno *see* (ona). Ukitumia neno *see*, unaweza kumaanisha "eneo la maji, nasikia," ama mambo mengi. *Bored* (chimba), "kuchimba shimo, kutengeneza barabara," ama—ama "you bored me (ulinichosha)" ama "you paid my board (ulinilipia malazi)," ama lingeweza kumaanisha

cho...mambo mengi. Na vokali hizo ndogo, na kadhalika, zinabadilisha maana yote. Kwa hiyo kamwe hutalifanikisha namna hiyo. Mungu aliliandika namna hiyo, kwa sababu...

122 Na Neno lote limevuviwa, Naye alisema ya kwamba, "Nakushukuru, Baba, ya kwamba umewaficha mambo haya kutoka kwenye macho ya wenye hekima na akili ukawafunulia" (amina) "watoto wachanga wanaoweza kujifunza." Ni ufunuo Wake, kama nilivyosema jana jioni, "Atawafunulia watoto wachanga."

123 Nikasema, "Haitafaa kitu, bwana." Nikasema, "Ufufuo hautakuja kamwe mpaka Mungu, mwenyezi Mungu, autume; ndipo basi anaweza kumchukua maskini mjinga fulani ambaye hata hawezi kuandika jina lake, na kutenda kazi pamoja naye, ambaye hata hajui Kiingereza kizuri sembuse Kiyunani."

124 Hivyo ndivyo alivyofanya wakati Petro alipohubiri siku ya Pentekoste, unajua, hata hakuweza kuandika jina lake, asiye na maarifa na asiye na elimu. Lakini Mungu hufanya mambo kwa njia ya ajabu sana kwa kuwazia kwetu kiakili. Hilo hulifanya kuwa ni Mungu. Kama angalichukua kundi la wanatheolojia na watu mashuhuri, na kadhalika, wangesema, "Yule Kayafa mwenye bongo, unaona, alilipata vizuri kabisa." Lakini Mungu alishuka akaenda akawachukua wavuvi ambao hawakuweza hata kuandika jina lao, na hao ndio aliowachukua. Huyo ni Mungu, huchukua kitu ambacho si kitu na kufanya kitu kutokana na hicho kwa utukufu Wake Mwenyewe. Alichukua mchafuko na akafanya Edeni. A-ha, ni Mungu.

125 Sasa, kama kuna mtu aliye na mitambo kwa ajili ya ufufuo, ni ndugu yetu wa heshima, Billy Graham. Lakini mitambo ni sawa, lakini mitambo haitauendesha, inahitaji nguvu za kuendesha upate kwenda. Unaweza kuunda motokaa, uweke viti vizuri ndani yake, pistoni nzuri na—na uthibitishe kwa sayansi vile unavyoweza kufanya; lakini isipokuwa nguvu za kuendeshea ziwemo, hilo ni bidhaa iliyokufa tu.

126 Kwa hiyo, katika uamsho wa Wesley, mmoja wa ufufuo wetu uliopita kabla ya ufufuo wetu wa Kipentekoste, hakuna aliyejua kilichouanzisha ufufuo huo, ni kundi tu la watu.

127 Sasa, tutakapopata yote...rafiki yetu, Billy Graham, atawakusanya Wapresbiteri wote, na Waluteri, na Wapentekoste, na kila kitu pamoja, aende mjini na huko watakuwa na kusanyiko kubwa la maelfu, na elfu thelathini watakuja (katika majuma mawili) na kumpa Kristo moyo wao; unarudi majuma mengine mawili wala huna hata mmoja. Unaona, hiyo ni mitambo. Lakini hebu Mungu katika neema Yake kuu anene tu na maskini mjinga fulani, tuseme, mtu ovyo; aruhusu Roho Wake ashuke mjini wala hakuna mtu anayeweza kufanya kazi, wanawake hawawezi kuosha vyombo, mjakazi hawezi kutengeneza kitanda, wanapiga makelele na kulia huku mikono

yao iko juu hewani. Huo ni ufufuo, huo uko katika mapenzi ya Mungu.

128 Ilisemekana ya kwamba watu mashuhuri kutoka kanisani walienda huko Wales wapate kuelewa, ama kuangalia mtambo mzima wa ufufuo huo ulikuwa ni nini, katika ule ufufuo wa Welshi. Na wakati walipotoka kwenye meli na makofia yao marefu, na kosi zao zimepinduliwa; wakamwona maskini polisi mmoja akishuka barabarani, akizungusha-zungusha fimbo yake namna *hiyo*, anapiga mbinja; wakasema, "Muungwana, je! unaweza kuniambia mahali ufufuo wa Kiwelshi ulipo?"

129 Akasema, "Naam, ndugu zangu, mmesimama katikati yake!" En-he, en-he, en-he. Akasema, "Mwajua, mimi ni ufufuo wa Kiwelshi, kwa kuwa ufufuo wa Kiwelshi umo ndani yangu mimi."

130 Hilo ni uweza! Hivyo ndivyo Mungu anavyofanya, na Yeye peke Yake ndiye aliye na haki ya kutuma ufufuo. Si kuunganisha mitambo, ni kuomba Mungu atume nguvu—nguvu za kuendeshea.

131 Yeye hufunua Neno Lake tu kwa waliochaguliwa tangu zamani. Sasa, ninapotumia neno *kukusudiwa tangu zamani* . . . Sasa, ni neno baya la kutumia hadharani, hasa sana wakati tunapokuwa na makundi yaliyochanganyikana kati ya Waamenia na Wakalvini. Wala si . . . Nimewaomba msifikirie mimi ni mjuvi, lakini wote wawili wamekosea kulingana na Maandiko. Neema ni yale Mungu aliyonitendea, kazi ni yale ninayomfanyia Yeye. Mnaona? Hapo ndipo umelipata. Kama ukipanda moja ya matawi hayo, hakika utajikuta kwenye ncha ya hilo tawi wala huwezi kurudi. Kitabu cha Waefeso kinakusanya hayo pamoja, nafikiri.

132 Sasa, lakini neno hilo, ninapolitumia, *kuchaguliwa tangu zamani*, msifikiri ya kwamba ninaninii . . . hilo ndilo neno tu ninalojua jinsi ya—ya kulifanya . . . Ni kujua kwa Mungu tangu zamani, unaona, kwamba Yeye alijua. Ha—hawezi kusema . . . A—alikufa ili wote wapate kuokolewa, alikufa, bali kwa kujua kwake tangu zamani Yeye alijua ni nani angeokolewa na ni nani asingeokolewa. Unaona? Hayo ndiyo yale anayojua, mimi sijui wala wewe hujui, kwa hiyo tunatimiza wokovu wetu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka.

133 Sasa, lakini Mungu ameweka Neno Lake, na ameliweka katika nyakati zote. Kujua Kwake tangu zamani kumemfanya aweke kanisani, na katika watu, mambo fulani aliyofanya tangu mwanzo. Halafu Injili inayohubiriwa kwa wakati *huo* inafunuliwa tu kwa watu fulani, hao wengine hawalioni. Unaona? "Nakushukuru, Baba, umeyaficha mambo haya machoni pa wenye hekima na elimu, ukawafunulia watoto wachanga wanaoweza kulifahamu." Unaona, huko ni kuchaguliwa tangu zamani. Si kwamba alifanya jambo hilo

kwa, unasema, "Nitakuchagua wewe, bali wewe sitakuchagua." Kwa kujua Kwake tangu zamani, Yeye alijua utakachofanya.

134 Kwa kuwa Yeye hana kikomo. . . Unaamini Yeye hana kikomo? Kama ana kikomo, Yeye hawezi kuwa Mungu. Basi, unawazia, kwa kuwa hana kikomo: Yeye alijua kila kiroboto atakayekuwa duniani, kwamba ni mara ngapi hao viroboto wangepepesa macho yao, ni shahamu kiasi gani yaliyokuwako katika kila kiroboto, kila jani la nyasi ambalo angeketi juu yake; huko ni kutokuwa na kikomo. Sisi tuna kikomo, tunagaagaa gizani. Mungu alitulinganisha na kondoo, na hatuna budi kuwa na kiongozi. Na kiongozi huyo si mwanadamu, kiongozi huyo ni Roho Mtakatifu, Roho wa Kristo kati yetu. "Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena." Mwili Wake wa kawaida uliinuliwa hadi kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu, ambapo Roho *alikuwa* juu ya Kiti cha Enzi; sasa Kristo yuko kwenye Kiti cha Enzi, Yesu. "Bado kitambo kidogo na ulimwengu haunioni tena, hata hivyo ninyi mtaniona, kwa maana nitakuwa pamoja nanyi hata ukamilifu wa dahari, hata ndani yenu." Kiti cha Enzi cha Mungu, cha Kristo, kimewekwa moyoni mwako; Naye ameketi kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu, lakini katika ule Utawala wa Miaka Elfu Yeye ataketi kwenye Kiti Chake Mwenyewe cha Enzi; ambapo, Yeye aliapa ya kwamba angemwinua mtu huyu, Mwanawe, Mwana wa Daudi, aketi kwenye Kiti Chake cha Enzi.

135 Sasa, Yeye hufunua mambo kwa kujua Kwake tangu zamani kwa hao ambao Yeye amewachagua kwa ajili ya mambo haya, la sivyo hawalioni. Wanasimama pale pale, wakiliangalia, wala hawawezi kuliona.

136 Ni wangapi waliopata kuona ile picha ya ng'ombe kichakani, ambapo inakubidi kuangalia na kuangalia? Je! mlipata kuiona? Ama, kuona picha ya Kristo kichakani, ama mbinguni, ama mawinguni? Unaona, mwanasanaa huyo ameitengeneza hivi kwamba inakubidi kuiangalia kwa njia fulani. Vema, basi, mara unapoiona, huwezi kuona kitu kingine ila hiyo. Kila unapoangalia, hiyo hapo. Ni wangapi wameshaona picha hizo? Vema, hakika mmeziona.

137 Vema, hivyo ndivyo Kristo alivyo, Yeye Mwenyewe, Injili, Ujumbe ulivyo. Mara unapouna Ujumbe wa wakati huu, hakuna kitu kingine unachoweza kuona ila Huo. Basi. Vitu vingine vyote vinatoweka, vilivyosalia ni kijazio tu (unaona? unaona?) mara unapoona Ujumbe!

138 Hivyo—ilikuwa hivyo katika wakati wa Nuhu. Wakati Nuhu na kundi lake. . . ona jinsi. . . Wakati walipoona Ujumbe huo, hawakujali jambo lingine. Wakati kundi la Musa walipouona, hawakujali jambo lingine. Wakati kundi la Yohana walipouona, hawakujali jambo lingine. Wakati kundi la Yesu walipouona, hawakujali jambo lingine. Wakati kundi la mitume walipouona, hawakujali jambo lingine. Wakati kundi la Luther walipouona,

kundi la Wesley walipouona, kundi la Kipentekoste walipouona, hawakujali jambo lingine, waliacha kila kitu. Kwa nini? Kwa kutangulia Kwake kujua Yeye aliyachagua tangu zamani mambo haya kutukia.

139 Yeye hujichagulia mtu Wake mwenyewe kwa kujua Kwake tangu zamani. Kama alivyosema katika Warumi 8 hapa, ya kwamba Esau . . . ya kwamba ku—kuchagua kwa Mungu kupate kusimama imara. Ya kwamba Esau na Yakobo wote wawili walizaliwa na wazazi watakatifu, mapacha, ili kwamba kuteua Kwake kupate kusimama imara na kuwe ni kweli, Yeye alisema, "Ninamchukia Esau, na ninampenda Yakobo," kabla hata mmoja wa hao wavulana kuzaliwa. Unaona? Yeye anajua kilicho ndani ya mwanadamu, alijua tangu mwanzo ilikuwa ni kitu gani, kwa hiyo Yeye anaweza kufanya kila kitu kitende kazi kwa wakati wake kabisa. Sisi huwa na wasiwasi sana na kuhangaikahangaika; hujapata kumwona Yeye akihangaika, hawahangaiki-hangaiki. Unaona? Kila kitu kinatenda kazi sawasawa, barabara kabisa, saa inasonga mbele.

140 Mambo haya yanayopaswa kutendeka, wanawake hawa wote wenye nywele fupi, na hawa wanaume wanaovalia ninii zao . . . walio na nywele kama za wake zao. Ninawaona, hakika, wana hizi rola za kutilia mawimbi nywele zao, wanaziweka mawimbi hapa mbele. Ni upotovu wa jinsi gani! Hayo ni matokeo ya Edeni ya Shetani. Pia angalia . . . ? . . . Anajaribu kukata nywele zake kama mumewe. Mumewe anaachilia nywele zake zikue kama za mkewe. Naye mwanamke anavaa nguo za mwanamume, naye mwanamume anavaa nguo za ndani za mwanamke. Unaona, haya basi. Mwanamke anakuwa kama mwanamume, naye mwanamume anakuwa kama mwanamke. Unaona, ni Edeni ya Shetani, kinyume na vile Mungu alivyoumba hapo mwanzo. Hiyo ni Kweli.

141 Kama sitaanza, hatutafikia jambo hili kamwe. Lakini mambo haya, na jinsi Yeye anavyopaswa kuyafanya, na kwamba ni nani atakayeyafanya, hiyo ni njia Yake Mwenyewe aliyoichagua, Yeye huchagua. Hivyo ndivyo anavyotaka ifanyike.

142 Kama nilivyomsikia Ndugu Pearry Green, mchungaji wetu huko Tucson, akihubiri hivi majuzi usiku juu ya jinsi Mungu alivyofanya vitu namna fulani (ninasahau somo lake lilikuwa ni nini), lakini alisema, "Hivyo ndivyo Mungu anavyotaka iwe, hivyo ndivyo anavyolifanya." Vema, hiyo ni kweli.

143 Sasa, ni nani kati yetu atakayemwambia, "Amekosea"? Ni nani angethubutu kusimama mbele ya uso wa Mungu, na kusema, "Umekosea, Bwana, inakupasa kulifanya jinsi ninavyotaka lifanywe, jinsi Dk. *Fulani* alivyosema linapaswa kufanywa"? Ni nani huyo ambaye amerukwa na akili sana,

kusema jambo kama hilo? La, hungetoka na kusema hivyo, bali unawazia!

144 Kama vile katika Ujumbe wangu wa *Mpinga-Kristo*, "Watainuka makristo wa uongo." Sasa, Yeye hakusema *Mayesu* wa uongo. Unaona, hakuna mtu angeweza kuvumilia kuitwa "Yesu," ikimaanisha Bwana. Lakini *makristo* wa uongo maana yake ni "waliopakwa mafuta."

145 Loo, wao, kila mmoja anafikiri wamekwisha kutiwa mafuta, "Mungu atukuzwe, yeye anaweza kufanya *hivi* na kufanya *vile*!" Lakini muweke kwenye jaribio la Neno uone atatokea wapi, unaona, kwenye Ujumbe wa wakati huu.

146 Walikuwa na upako katika wakati wa Yesu, lakini si Wake.

147 Walikuwa na upako wakati. . .Hata Dathani alikuwa na upako wakati wa Musa. Alisema, "Sasa, usije ukafikiri wewe ndiwe tu uliye mtakatifu kati yetu, Mungu ana wengi. Tutaunda tu madhehebu hapa, kundi la watu."

148 Mungu alimwambia Musa, "Jitenge naye," ndipo akafungua nchi ikawameza. Alikuwa amempa Musa Neno Lake la asili, nabii Wake; hiyo ndiyo njia pekee aliyowahi kufanya jambo hilo, na njia pekee atakayowahi kulifanya. Yeye habadilishi mpango wake, unaona.

149 Kwa hiyo mawazo yetu si sahihi, mawazo Yake ndiyo sahihi, daima. Wala usijaribu kumwambia ya kwamba Yeye "amekosea." Haidhuru ni nani tunafikiri anafaa kuliko wote, si juu yetu kusema ni nani anafaa kuliko wote. Sasa, hapo ndipo unapoingia katika madhehebu yako.

150 Maskini ndugu fulani aliyejazwa na Roho ataenda katika mji fulani na kuunda madhehe-. . .aunde kundi zu—zuri la watu, nao watakutana mkutanoni, na ndugu wote watakatifu watakuja, unajua, na kusema, "Wajua nini? Ninaamini maskini *Jones* hapa," (yeye kidogo ni mashuhuri miongoni mwao) "Nafikiri anapaswa kupata ile maskani nzuri kubwa, nafikiri. Huoni hilo ni sawa?" La, jamani. Huyo hapo anakwenda. Ndipo kusanyiko linatawanyika. Unaona? Watenganishe hawa! Mungu ndiye anayetenganisha, Yeye ndiye anayefanya hivyo. Lakini hao wote, kila mmoja, anataka kumchukua maskini jamaa *huyu*, amweke hapa, na *huyu* amshushe chini. Hilo ni wazo la mwanadamu.

151 Mwanadamu ana funguo, lakini kwa kweli Mungu ndiye aliye na hizo funguo. Waliwapa wanafunzi, kanisa takatifu, zile funguo; basi angalia mara ya kwanza walipoutumia, wakati Yuda alikuwa ameanguka kwa uasi. Walikusanyika wakapiga kura, na hao ndugu watakatifu. . .(ni nani angesema hawakuwa ndugu watakatifu? ni nani anasema hawakuwa watakatifu?). Lakini walipiga kura, nayo ikamwangukia Mathia. Na wakati yeye. . .Aliwahi kufanya nini? Hakuna. Lakini Paulo ndiye aliyekuwa ameteuliwa! Amina. Hilo lilikuwa ndilo chaguo la

Mungu: Myahudi mdogo, mwenye pua iliyopindika, mchokozi, mwenye hasira kali. Si yule Mathiya, ile D.D., unajua, ye—yeye alikuwa . . . Lakini Paulo, Mungu alimchagua Paulo; kanisa likamchagua—likamchagua Mathiya. Unaona? Huna haki ya kumwambia Mungu kwamba "amekosea." Anajua la kufanya, Yeye anajua mtu amefanywa kwa kitu gani.

152 Ni nani angeweza wakati wo wote . . . Kanisa hilo lingewezaje kumchagua Paulo? Loo, la, hata kidogo. Kasema, "Jamaa huyo ndiye anayetutia sote gerezani."

153 Lakini Mungu alisema, "Nitamwonyesha yatakayompasa kuteswa kwa ajili Yangu." Atajua nini.

154 Vema, haidhuru ni nani tunayemdhania kwamba yuko sawa, Mungu anajua ni nani anayestahili kuliko wote kwa maana Yeye anajua moyo wa mwanadamu, Yeye anajua.

155 Wala ufufuo, au mambo haya, yanatukia wakati tunapofikiri yatatukia. Tunafikiri, "Ni wakati huu sasa hivi, Mungu atukuzwe!" Ninaona katika matawi yetu na kadhalika ya Wafanyi Biashara, "Kunakuja sasa hivi, haleluya, ufufuo mkubwa!"

156 Msidanganyike, "Amekwisha kuja, nao wakamtenda waliyotaka." Mnaona? Lakini wao wanafikiri kuna ufufuo. Unatokea? La! Umekwisha, na umekufa, umeisha. A-ha. Angalia, huu ni wakati wa kutengeneza taa, kutoka na kuingia. "Wamngojeao Bwana watapata nguvu mpya."

157 Angalia hapa katika kifungu chetu, angalia Daudi, mfalme wa Israeli, ndiye aliyepata ufunuo wa kurudisha sanduku la Mungu mahali pake; ambapo, hawakuuliza neno kwa hilo katika siku za Sauli maana Sauli alikuwa ameanguka. Kwa hiyo hawakutaka shauri kuhusu hilo sanduku hata kidogo, lile agano, katika siku za Sauli, kwa kuwa alikuwa amerudi nyuma na kuenda mbali na Mungu. Kwa hiyo Daudi, upesi, kwa uvuvio . . . Sasa angalia jambo hili, ni somo linalotatiza sana usipolifahamu vizuri. Nami ninahisi ya kwamba saa yaja ambapo tunapasa kuwa watu wazima badala ya watoto wachanga. A-ha. Tunapaswa kula chakula kigumu badala ya maziwa.

158 Angalia Daudi, mfalme wa Israeli, mfalme alikuwa ndiyo kwanza tu atiwe mafuta awe mfalme; ama kuchaguliwa kuwa mfalme, Sauli . . . Samweli alimtia mafuta kwa mapenzi ya Mungu; naye alikuwa kabisa ni Mfalme aliyechanguliwa na Mungu, hakuna shaka juu ya hilo. Na ndiye huyu hapa, na uvuvio ukamgusa. Likafunuliwa kwa Daudi. Alipata ufunuo huo, hakuna mtu mwingine aliyekuwa amesema kitu juu yake. "Hebu twende tukalichukue sanduku, maana hayo ni mapenzi ya Mungu kwamba tuwe na sanduku hili hapa, tupate kumtaka shauri Mungu kwa sanduku hili." Jambo zuri sana, sana. Sivyo? Vema.

159 Kumbukeni, lakini, yeye akiwa mfalme, na kupokea ufunuo, alitoka mahali pake. Kulikuwako na nabii nchini jina lake Nathani, yeye ndiye aliyechaguliwa apate ufunuo. Kukiwapo na cho chote cha kunenwa, Yeye alisema, "Bwana hatendi neno lo lote mpaka awafunulie watumishi Wake nabii." Lakini, unaona, Daudi akiwa ni mfalme, akiwa na upako juu yake. . . Sasa, hayo ni Maandiko? Akiwa ametiwa mafuta, na ana ufunuo wa kweli; lakini lilikuwa ni kosa. Kwa sababu Nathani alikuwa ndiye nabii wa wakati ule, wala ufunuo haukumjia Nathani, na wakati ufunuo ulipomjia Daudi yeye hata hakumtaka shauri Nathani kuhusu hilo. Ataendelea na kufanya yale aliyotaka kufanya, a-ha.

160 Lakini angalia Daudi alifanya shauri na akina nani hapa katika mlango wa 13, "Lakini akafanya shauri na maakida wa maelfu na wa mamia," akarudi kwenye kusanyiko lake. Unaona? "Sasa, je! hamwoni kwamba tunapaswa kunininii. . .?" Hivyo sivyo. Sasa, yeye alikuwa akijaribu kumfanyia Mungu kazi, lakini hakuwa amechaguliwa kuifanya; unaona, maana Mungu alikuwa na njia yake.

161 Sawasawa na vile Mungu angeweza kunena na m—mfalme juu ya kidonda chake na kupata afya, lakini Yeye hakufanya hivyo, alikuwa na njia aliyoandaa ya kufanya jambo hilo, huyo alikuwa ni nabii Wake. Kwa hiyo akanena na nabii. Isaya alimwambia arudi akamwambie Hezekia lile litakalotukia.

162 Sasa, Hezekia alikuwa akizungumza uso kwa uso na Mungu, na—na Mungu aliweza kunena na Hezekia, bila shaka, lakini alifanya njia fulani! Mnafahamu jambo hilo? Mungu ana njia Yake Mwenyewe iliyoandaliwa ya kufanya mambo: kutuma ufufuo, kuzungumza, kunena, cho chote kile. Ana njia Yake ya kufanya jambo hilo, nasi si watu wa kumwambia jinsi ya kulifanya. Yeye hulifanya jinsi inavyompendeza kulifanya.

163 Kwa hiyo, unaona, Daudi, akiwa amevuviwa. . . Sasa, mnakumbuka nilisema kule kutiwa mafuta, kutiwa mafuta ya uongo? Kumbuka Roho Mtakatifu anaweza kuja na kumtia mafuta mtu, na hata hivyo ni nje ya mapenzi ya Mungu. Hapa, inathibitisha jambo hilo papa hapa. Unaona? Hatuna budi kupitia katika njia ya Mungu ya kufanya jambo hilo, si njia zetu, njia ya Mungu ya kufanya jambo hilo. Maana, Daudi, akiwa ni mfalme, ametiwa mafuta, ametiwa mafuta na Roho wa Mungu juu yake (mfano wa Yesu Kristo), lakini hiyo haikuwa ni njia ya Mungu.

164 Wakati kusanyiko lote, "jambo hilo liliwapendeza," Biblia ilisema. Angalia, maakida wa maelfu na wa mamia, pia makuhani na wanatheolojia walidhani hilo lilikuwa ni "zuri sana." Hizo hapo shule zenu za Biblia na cho chote kile, wao walidhani ilikuwa ni "zuri sana." Hata watu wote wakakubali, na makuhani, na—na wote walikubali ya kwamba upako wa

mfalme ulikuwa ni sawa. Angalia! Lakini Mungu hakuwa ameahidi kufunua Neno Lake katika wakati Wake *kwao*. Mungu alikuwa na njia Yake ya kufunua Neno Lake, lakini si *kwao*. Kumbuka, ilikuwa ni kinyume cha Mungu.

165 Kitu kama katika siku za Mika mwana wa Imla. Je! mnakumbuka hadithi hiyo? Yuda na Israeli walitengana, nao walikuwa na falme mbili mbalimbali, naye Ahabu alikuwa ni mfalme wa ufalme mmoja. Na Yehoshafati alikuwa mfalme wa ufal—ufalme wa Yuda, ninaamini ndivyo ilivyokuwa; naye Ahabu alikuwa juu ya Israeli, Yerusalemu.

166 Angalia, halafu hili hapa kundi la wageni likaja na kuchukua sehemu ya nchi waliyopewa na Mungu ambayo Mungu alikuwa amewapa Israeli, na Wafilisti hawa hapa juu, Waashuri, walikuwa wameliteka eneo hilo nao walikuwa wakiwalisha watoto wao kutokana na ardhi iliyokuwa ni mali ya Israeli. Na kwa hiyo walihitaji eneo hilo wapate kuwalisha watoto wao na jamaa zao wenyewe. Mungu aliwapa . . . Hizo zilikuwa ni haki zao walizopewa na Mungu.

167 Na kwa hiyo Ahabu akamwita Yehoshafati, na kusema, “Shuka uje.” Akasema, “Angalia kule jinsi adui wetu anavyofanya. Ni haki kwamba sisi, watu wa Mungu, tukiwa na haki tuliyopewa na Mungu kwamba tunapaswa kuwa na nchi hii, ni yetu, Mungu kupitia kwa nabii wake, Yoshua, aliigawa nchi hii, inapaswa kuwa ni yetu; ni mali yetu sisi, ni ya watoto wetu, na hapa wakomunisti wameichukua, nasi tunaninii . . . Tuna njaa sana, nao wana haki zetu tulizopewa na Mungu. Je! hudhani tunapaswa kupanda kwenda kule na kuitwaa nchi yetu tuirudishe? Kama utakusanya jeshi lako: kama ninyi Wamethodisti, na Wapresbiteri, na ninyi nyote, na Wapresbiteri, na Waluteri, na kadhalika, nyote mkichukua baraza la ekumeni hapa sasa, sisi sote tutaketi pamoja, nasi tutakitwaa kitu hicho.” (Ninasema na kuzungumza kwa njia ya mfano sasa) “Tutaenda tukaitwae.”

168 “Mbona,” akasema, “bila shaka, sisi sote ni mmoja.” A-ha.

169 Sasa, Biblia ilisema, “Watu wawili wawezaje kutembea pamoja wasipokuwa wamepatana?” Unaona?”

170 Hapo ambapo huyo mtu mashuhuri, huyo mtu mashuhuri wa Kipentekoste, Yehoshafati, alijichanganya na kusanyiko baya. Na hivyo ndivyo ilivyotendeka kwa Wapentekoste wetu leo. Kuna watu wanyofu kule, lakini wamechanganyikana katika kundi hilo la kimadhehebu. Ondokeni kwenye kitu hicho! Kimelaaniwa na Bwana!

171 Angalia sasa! Huyo hapo, naye akasema, “Naam, hilo linasikika kuwa la maana.” Kasema, “Kanisa letu liko hapa, ni watu wetu; hata hivyo, sisi sote ni Wayahudi.” A-ha. “Hakika, tutakwea pamoja nanyi.” Lakini kulikuwako na dini ya kutosha iliyosalia katika Yehoshafati kusema, “Je! huoni inatu—

inatupasa kumtaka shauri Bwana kwanza?" Unaona? "Nafikiri lingekuwa ni wazo zuri."

172 Mbona, Ahabu, "Bila shaka." Kasema, "Mbona, loo, hakika, nilipaswa kuwa na wazo hilo."

173 "Vema, je! kuna mtu wa Mungu mahali fulani? Je! mna nabii?

174 "Aha, hao ninao mia nne. Nina baraza zima hapa, madhehebu yote. Wao ni manabii wa Kiebrania."

175 Sasa kumbukeni, Biblia ilisema walikuwa ni "*manabii*, manabii wa Kiebrania," si manabii wa kipagani, manabii wa Kiebrania; shule nzima, seminari ya kitheolojia.

176 "Vema, walete!"

177 Nao hao wafalme wakavaa na kuketi mbele yake ili kumvutia nabii. Naye huyu hapa anakuja, ninaamini Zedekia ndiye aliyejitokeza, kiongozi mkubwa wa wajumbe wa wilaya, ama cho chote alichokuwa, akaja pale miongoni mwao. Akajifanyia pembe mbili kubwa, akasema, "Nimesikia kutoka kwa Mungu. BWANA ASEMA HIVI, 'Kwa pembe hizi utawasukuma Waashuri moja kwa moja kutoka nchini.'"

178 "Loo utukufu!" kila mtu alifikiri hilo lilikuwa ni zuri sana, sawa.

179 Angalia jinsi inavyokaribia kwenye makali hayo ya wembe sasa, kati ya kweli na uongo. Na kumbuka itaangukia upande mmoja ama huo mwingine, mpaka wakati mwingine inakuwa kama wembe mkali baina ya tafauti kati ya kweli na uongo. Haina budi kuwa ni kila Neno la Mungu; si karibu tu kila Neno, lakini kila Neno! Na imefikia ambapo leo, si kwa Waluteri, si kwa Wamethodisti, si kwa Wapentekoste, lakini kwenye wakati huo ulionolewa, katika wakati huu ambapo upako wa mpinga Kristo ni mkamilifu sana, hata ingewapoteza walio Wateule, wataangukia upande mbaya kama hawakuangalia jambo hilo, kama kabari. Angalia! Iweni waangalifu! Hatuishi katika wakati wa Kipentekoste sasa. Tumepita wakati huo, kama tu vile tumepita wa Kiluteri, na kupita . . . Unaona?

180 Angalia. Sasa manabii wote walitabiri, hao mia nne, manabii wa Kiebrania, waliolishwa vizuri, wamevalishwa vizuri, wakashuhudia, kwa moyo mmoja, "BWANA ASEMA HIVI, 'Kweeni, Bwana yu pamoja nanyi.'"

181 Yehoshafati akasema, "Vema, hilo—hilo linaonekana kuwa ni sawa. Lakini," akasema, "Je, una mwingine?"

182 "Mwingine? Tuna madhehebu yote hapa, baraza lote tunalo limekusanyika hapa. Kwa nini tuhitaji mwingine?"

183 Akasema, "A-ha," kasema, "nilifikiri labda huenda kulikuwako na mwingine."

184 Akasema, “Loo, naam, yupo mwingine, lakini yeye hata si wa baraza hili.” A-ha. “Huyo ni mtu aliyetengwa. Ni Mikaya, Mwana wa Imla, nami ninamchukia.” Unaona? Kasema, “Wao hawatampokea katika ushirika, naye kwanza ni mtu wa kawaida aliyetengwa na jamii. Naye daima, kila analotabiri, yeye hata hataitia moyo seminari yangu.” A-ha. “Naye hufanya mambo yote haya maovu, yeye sikuzote ananitabiria mabaya, ili kwamba tu eti awe ni tofauti.

185 “Loo, Yehoshafati akasema, “mfalme na asiseme jambo kama hilo. Lakini ningetaka kusikia ambalo mtu huyu anasema.”

186 Kasema, “Vema, tutampata.” Kwa hiyo wakatuma mahali fulani jangwani, nao wakamtuma mtu.

187 Akasema, akamwambia, akasema, “Sasa, wakati ukirudi sasa, ninataka kukwambia jambo fulani. Je! unataka kurudi kwenye madhehebu tena?” Unaona? “Je! unataka kuwa na ushirika na watu wote tena? Kama unataka, sema neno lile lile mzee wa kanisa wa jimbo analosema, sema neno lile lile askofu analosema, nao watakurudisha moja kwa moja. Sasa huu ndio wakati wa kufanya jambo hilo.”

188 Lakini je! ungeweza kuwazia nabii wa kweli wa Mungu, aliyetiwa mafuta akipatana katika Neno moja la Mungu? La hasha!

189 Akasema, “Kama Bwana aishivyo, nitasema tu yale Mungu anayosema!” Tunahitaji mwana wa Imla. “Kama Bwana aishivyo, nitasema tu yale Yeye asemayo.” Hiyo ni kweli, “Yale *Yeye* asemayo.”

190 Kwa hiyo walipoenda kule mbele za watu, manabii wote, wakasema, “Sasa, wewe useme . . . ”

191 Akasema, “Ngoja, nipeni usiku wa leo, hebu nione Bwana atakalosema.” Kwa hiyo, usiku ule, Bwana akamtokea katika ono na kumwambia atakalosema.

192 Kesho yake asubuhi akasema, “Unasemaje, Imla?” wakati hao wote walipokuwa wamesimama huko nje . . . Ninamaanisha “Mikaya, mwana wa Imla,” kasema, “unasemaje sasa? Sote tuko hapa pamoja, makuhani wote, na manabii wote, na wafalme wote, na kila kitu kiko hapa vizuri. Wasemaje sasa mbele ya baraza hili kuu?”

193 Kasema, “Kweeni,” kasema, “lakini niliona Israeli wametawanyika kama kondoo wasio na mchungaji.”

194 Ndipo Ahabu akasema, “Je! nilikwambia nini! Msaliti huyo anachoweza tu ni kutabiri maovu juu yangu!”

195 Angewezaje kusema jambo lingine wakati Mungu alikuwa anasema jambo lile lile? Nabii anapaswa kuwa ni kinywa cha Mungu kikinena, si mawazo yake mwenyewe. Ninii yake . . . Unaona, yeye kabi- . . . amejisalimisha kabisa kwa Mungu, hata

hataki kudhuru kitu cho chote, lakini inambidi kusema vile Mungu anavyosema, maana yeye mwenyewe hana amri juu ya jambo Hilo. Unaona?

196 Akasema, "Sasa, si nilikwambia?"

197 Ndipo akaja mtu m—mkubwa akiwa na pembe, akampiga kofi mdomoni, akasema, "Roho wa Mungu alipitia wapi wakati alipotoka kwangu?" Kwa maneno mengine, hebu nijaribu kupanua jambo hilo, "Angalia hapa katika. . . Angalia hapa, ninataka kukwambia jambo fulani, Mikaya. Je! unatambua ya kwamba mimi ni hodari katika Maandiko? Je! unatambua ya kwamba mimi nina upako?" Ama, "Ubatizo," tungesema hivyo siku hizi. "Je! unatambua ya kwamba nina huo?"

198 Imla akasema, "Sitilii shaka hilo."

199 Akasema, "Lakini sikiliza! Roho wa Mungu ameniambia, na kushuhudia kwa hawa mia nne wangu hapa, ya kwamba 'tutawasukuma Waashuri watoke nchini.' Basi wewe ni nani wa kuja hapa na kusema ya kwamba mfalme wetu mkuu atauawa?" Akasema, "Roho wa Mungu aliniambia hivyo."

200 Hebu nilifafanue tu ili mpate kulifahamu. Na labda tunamwona Mikaya akisema, "Jana usiku katika ono, bwana, nilimwona Mungu ameketi juu ya Kiti cha Enzi. Kisha nikaona majeshi yote ya Mbinguni yamemzunguka, a-ha, nao walikuwa wakifanya baraza Mbinguni. Wakasema, 'Ni nani tunaweza kumtuma ashuke aende akamdanganye Ahabu? Kwa maana chini ya Kiti cha Enzi hapa kuna nabii, nabii wa kweli, jina lake ni Eliya. Naye ametabiri kwa Neno Langu na kusema ya kwamba "Huyo Ahabu mwovu, kwa kuwa alimwua Nabothi, mbwa watairamba damu ya mtu huyo mwovu," Nasi hatuna budi kutimiza jambo Hilo kwa kuwa tayari limenenwa tayari, ni BWANA ASEMA HIVI! Halina budi kutimia, halina budi kuwapo. Nasi tutafanyaje jambo hilo?'"

201 "Ndipo chini huko kutoka kwenye maeneo ya kutambaa ya waliopotea, huko chini kabisa akatokea roho fulani anapanda juu, akasema, 'Mimi ni mdanganyifu, na kama ninaweza kuwatumikia, nitashuka niende nikamwingie nabii wake.'" (kwa kuwa walikuwa wamejifunga sana katika madhehebu hivi kwamba wataelewa tu jambo moja, na hilo kidogo husababisha wasiwasi) "'Nami nitawafanya watabiri uongo. Nami nitamfanya Ahabu awasikilize hao watu mashuhuri badala ya nabii Wako wa kweli; maana atachunguza kila kitu anachosema kwa Neno Lako, atachunguza maono *yake* kwa Neno, atachunguza kila kitu anachofanya kwa Neno, na kama haliambatani na Neno hatalisikiliza. Lakini kama ni. . . Ninaweza kuwadanganya hawa wengine, nami nitaninii. . . wao. . . Ahabu ana matumaini makubwa sana katika huo mfungamano wa pamoja wa usalama wao, kwa hiyo wanaenda pamoja kila mahali nao wataungana. Nami nitamfanya Ahabu

kuwasikiliza, atoke aende kule. Na hivyo ndivyo tutakavyofanya jambo hilo.'"

202 "Mungu akasema, 'Unaweza kufanya jambo hilo, wewe ni mdanganyifu kweli; shuka uende kule.'"

203 Ndipo Zedekia akampiga mdomoni, kasema, "Ulikuwa wapi . . . ?"

204 Akasema, "Utajua wakati utakapokuwa umeketi kwenye chumba cha ndani." A-ha.

205 Akasema, "Kwea!" Zedekia akamwambia mfalme. Akasema, "Kwea na urudi kwa amani!"

206 Ahabu akasema, "Mchukue jamaa huyo ukamtie gerezani. Mfungeni pingu, mlisheni chakula cha shida na maji ya shida. Na wakati nitakaporudi na ushindi wangu kutoka hapa nje, ambapo manabii wangu wameniambia ya kwamba 'ufufuo huu hauna budi kutukia,'" kasema, "Jamaa huyo atanitambua!"

207 Sikilizeni maneno ya mwisho ya Mikaya kwa mtu huyo: "Ukirudi kabisa, basi Mungu hakunena nami." Loo!

208 Unaona, Mungu ana njia yake ya kufanya mambo. Watu hawa walidhani walikuwa wakimtumikia Mungu. Iweni waangalifu! Si mhemko, si shauku, si mawazo, lakini halina budi kuwa ni BWANA ASEMA HIVI," halina budi kuwa ni kweli. Vema, haidhuru . . . Tunaona mambo haya kwamba ni kweli.

209 Angalia sasa wakati Daudi alipokuwa ametoa tangazo hili kuu. Na lilionekana kana kwamba ni zuri, jambo zuri la kufanya, ingawa tunapata kwamba ninii . . . (je! ninawachosha? Je! nimechelewa sana kuwa na ninii nyingine . . . ?) Daudi alitoa tangazo hili kuu, hakumtaka shauri nabii.

210 Sasa, kila mtu anajua ya kwamba Amosi 3:7 inasema ya kwamba Mungu aliahidi ya kwamba hangefanya neno kamwe mpaka kwanza amfunulie nabii Wake. Kupitia kwenye nyakati za kanisa tumekuwa na watengenezaji; lakini aliahidi kwa Malaki 4 ya kwamba kungekuwako na nabii nchini katika siku za mwisho (kwa sababu haina budi kuambatana na mpangilio huo, unaona) kabla ya kuja kwa wakati wa misho.

211 Kabla ya kuja kwa kwanza kwa Yesu, Eliya alikuja, Eliya wa Malaki 3. Mathayo 11 inasema hivyo, "Kama mnaweza kufahamu hilo, huyu ndiye aliyenenwa habari Zake, 'Tanzama ninamtuma mjumbe Wa—Wangu mbele Zangu.'" Sasa, Yeye ametabiriwa, wanatheolojia wote wanaamini jambo hilo; ya kwamba, katika siku ya mwisho, Roho wa Eliya atakuja, pia. Hana budi kuja mara tano, Mungu anatumia Roho huyo: Elisha, Eliya, Yohana Mbatizaji, na kwa ajili ya kanisa la Mmataifa, halafu kwa Wayahudi katika Ufunuo mlango wa 11. Hiyo ni, n-e-e-m-a ya Mungu, i-m-a-n-i, J-e-s-u-s, Yesu, he—herufi

tano. Huwezi kusimama kwenye nne, haina budi kufikia tano. Unaona? Angalia!

212 Sasa, Yeye aliahidi jambo hilo, kwa hiyo hilo linaiweka Biblia kwenye siku hii hasa, na Sodoma na Gomora. Na Eliya hakuwa . . . Huyo hakuwa Eliya, huyo alikuwa ni Roho wa Mungu juu ya Eliya; Eliya alikuwa ni mwanadamu tu. Sasa, tumekuwa na akina Eliya, na makoti ya Eliya, na majoho ya Eliya, na kila kitu cha Eliya. Lakini Eliya wa siku hizi ni Bwana Yesu Kristo. Yeye anakuja kulingana na Mathayo kumi na sa- . . . Luka 17:30, inasema Mwana wa Adamu atajifunua Mwenyewe miongoni mwa watu Wake. Si mwanadamu, Mungu! Lakini itapitia kwa nabii. Sasa, kamwe Yeye hajawa na manabii wakuu wawili kwa wakati ule ule, kamwe, ulimwenguni. Unaona? Haidhuru ni jinsi gani kuna . . . viongozi wawili hawawezi . . . Haina budi iwe ni kiongozi mmoja. Mungu hana budi kumweka mtu mmoja chini ya mamlaka Yake. Unaona? Kuna Mungu mmoja; kulikuwa na Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, lakini Mungu mmoja juu ya yote, angalia, na alitumia tu ofisi hizo. Ndivyo amefanya na Eliya, Roho wa Eliya; Yeye alitumia Roho huyo, lakini ni Mungu yeye yule akiiongoza daima kutimiza Neno Lake.

213 Sasa, angalia katika jambo hili sasa, Daudi alifikiri alikuwa ameweka kila kitu katika utaratibu. Naye alikuwa amevuviwa. Unaona jinsi Roho Mtakatifu anavyoweza kumtia mtu mafuta? Lakini haina budi kuwa katika kanuni ya kutia mafuta. Roho ya nje inaweza kutiwa mafuta kwa Roho Mtakatifu, na nafsi ni nyeusi kabisa. Gugu linakua kwa maji yale yale yanayokuza . . . yanayoweka uhai katika ngano, yanaweka uhai katika gugu; lakini ndani kabisa ya gugu, ni uhai wa gugu. Linafurahi, na linachanua, lina uhai, na kufanya kila kitu ambacho ngano inafanya, lakini ile *nafsi* yake ni *gugu*. Unaona? Waalimu wa uongo wanaweza kuinuka, wakifundisha kila namna ya utatu na cho chote kile, na watiwe mafuta na Roho Mtakatifu, na wafanye miujiza mingi sawasawa na Injili ya kweli inavyofanya. Lakini kwa Neno hapa, hilo ndilo linayatenda mambo hayo. Unaona ninalomaanisha? Sasa, ni sawa kufundisha jambo hili, nadhani, mimi—mimi niko katika maskani ya madhehebu mbalimbali asubuhi ya leo, katika—katika hoteli hii hapa.

214 Angalia, angalia yale tunayosema. Sasa, vema, sikilizeni. Daudi alikuwa na mwamsho wote ambao ufufuo wa kweli ulikuwa nao. Angalia! Walipiga makelele, walipaza sauti, walicheza, kwa kweli walipata kitu fulani kutokana na upako huo. Hakika walifanya hayo! Yote kama tu ufufuo halisi, lakini, unaona, Mungu hakuwa ndani ya huo. Mungu hakuwa ndani yake. Alikuwa na nabii ameketi papo hapo nchini ambaye walipaswa kuwa wamemjua. Unaona? Daudi alipaswa kuwa amejua jambo hilo.

215 Ni jambo lile lile siku hizi, tuna mitambo yote, kama vile madhehebu makubwa, mikutano mikubwa ya wakati wetu,

lakini matokeo yake ni kama yale yale yaliyokuwako wakati huo; matokeo yetu ya mikutano yetu mikuu, na maana yetu kubwa na nzuri, majengo yetu makubwa, na ninii yetu kubwa . . . tunajenga maelfu, na kuongeza wafuasi na kadhalika, inatokea vile vile, yote ni bure. Sisemi jambo hilo eti niwe tofauti, ninasema jambo hili kusudi niwe mwaminifu mbele za Mungu Ambaye ninasimama karibu na Kitabu Chake asubuhi ya leo. Unaona? Yote yanatokea kuwa ni bure, matokeo yale yale.

216 Sasa hebu na tuone ilivyokuwa wakati Mungu (katika majira na wakati Wake) na manabii wake wanapopuuzwa, kutegemea tu theolojia, makasisi, umadhehebu kama tunavyofanya siku hizi. Sasa, kwa makini. Yote yanachafuliwa. Kama Roho wa kweli wa Mungu yuko, Yeye ataliongoza kwenye Neno; si mahali pamoja tu katika Neno, Neno lote kwa ajili ya wakati mzima. Unaona?

217 Siku ya Pentekoste, Roho alilielekeza moja kwa moja katika Hilo, kwenye Yoeli 2:38. Unaona? Siku za Luther, alilielekeza moja kwa moja kwenye Hilo; Wesley; katika mwenendo huu wa mwisho wa kipentekoste; lakini huu ni wakati mwingine, huku ni kuitwa kwa Bibi-arusi atoke. Si miaka elfu mbili iliyopita ile Siku ya Pentekoste, ama marudio, ama kurudia. Pentekoste . . .

218 Roho Mtakatifu alikuwa katika Luther, Roho Mtakatifu alikuwa katika Wesley; ni Neno la Mungu likitiwa mafuta. Naye Roho Mtakatifu akarudi kwa watu wa wakati huo nao wakaanza kuwa na kurudishwa kwa karama. Walikuta kwamba, kwa kujinyenyekeza wenyewe kwa Mungu, Roho Mtakatifu alinena kwa lugha kupitia kwao. Waliweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao wakapata afya. Walicheza katika Roho. Unaona? Huo ulikuwa ni wakati wa yale matengenezo ya kurudisha kanisa katika utaratibu. Na utaratibu wa mwisho wa kanisa ulikuwa ni kuweka karama kanisani; kama vile Luther alivyoweka kuhesabiwa haki, Wesley aliweka kutakaswa, Pentekoste ikaweka karama. Lakini wao walifanya nini? Kosa lile lile, kama vile maumbile yalivyolifananisha na ubua la ngano, waliunda madhehebu (ambayo yanapingana na Mungu, ni kinyume na Mungu.)

219 Sasa, tunaona ya kwamba wakati . . . Basi wakati hawa shina wanapojikusanya pamoja, wanaunda wazo lao wenyewe. Na haidhuru . . . Wakati lile “suala geni,” kama wanavyoliita, lilipotokea kwa Assemblies of God, wao walifanya nini? Hawangeweza kulipokea. Haidhuru ilikuwa ni Kweli jinsi gani, ubatizo katika Jina la Yesu Kristo, wao walikuwa tayari ni Baraza Kuu. Mwanadamu tayari alikuwa amechukua mamlaka, Roho alikuwa tayari amewaacha. Kabisa! Ndipo jambo hili likatokea . . . Nimezungumza na baadhi ya viongozi wenu walio bora sana; wao wanasema, “Vema, tungefanya nini sasa?” Wangejiaibisha. Wakati, wao wanajua kwamba ni Kweli; kama hawajui, wao ni vipofu kiroho na hawaijui Biblia. Si kwamba

nasema jambo hilo kwa chuki, sasa, nasema hilo kwa uchaji. Maana hakuna mahali katika Biblia ambapo mtu ye yote aliwahi kubatizwa kwa hutumia nyadhifa hizo, "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu." Wala haukutumika mpaka baada ya baraza la ekumeni, kanisa Katoliki la Kirumi. Katekisimo yao wenyewe inashuhudia jambo lile lile. Ni fundisho la sharti la Katoliki! Si fundisho la Biblia, bali ni fundisho la sharti la Katoliki. Na ninyi Wamethodisti mlitoa katekisimo yenu na kila kitu kama tu waliyokuwa nayo, mkitoka polepole tu. Na sasa mnapofikia kwa Wapentekoste, mkasambaza baadhi ya mafundisho hayo ya sharti, mliendelea tu kuyashikilia.

220 Lakini sasa ni kuitwa kwa Bibi-arusi, sasa ni wakati ambapo Mihuri Saba imefunguliwa, sasa wakati yale mambo makamilifu ambayo watengenezaji waliacha yatafunguliwa; na Malaki 4 tu ndiyo inayoweza kufanya jambo hilo, kwa sababu inachukua ufunuo wa moja kwa moja kutoka kwa Mungu hadi kwa mtu binafsi kufanya jambo hilo. Hiyo ni kweli! Hauwezi kulijia kundi, haijatukia kamwe. Mtu mmoja! Hivyo ndivyo Mungu alivyoahidi katika vivuli vya Yeye kuja kwa Bibi-arusi Wake, Eliezeri fulani. Unaona?

221 Angalia wakati makasisi, wahudumu na kadhalika, wanapopata uvuvio wao wenyewe, na wametiwa mafuta kwa hakika. Daudi alikuwa ametiwa mafuta. Biblia ilisema hivyo. Lakini, unaona, yeye alipitia katika njia mbaya, alipitia njia mbaya ya mawasiliano. Alipitisha upako wake upande mbaya, kwa watu na yale waliyofikiria, kwa maakida, yale waliyofikiria, badala ya kupitishia kwa njia takatifu ya Mungu apate kujua kwamba BWANA ASEMA HIVI inasema nini, "Je huu ni wakati wa jambo hili? Je! haya ndiyo majira yake? Je! haya ni mapenzi ya Mungu?"

222 Basi kama yeye ni nabii wa kweli wa Mungu, ataenda mbele za Mungu kwanza, aseme, "Baba, ni kitu gani?" kama vile Nathani alivyofanya baadaye kwa Daudi.

Daudi alisema, "Je! ni vizuri mimi kuishi katika nyumba ya mwerezi, na sanduku la Mungu wangu linakaa chini ya mahema huku nje?"

223 Na hebu mwangalie Nathanaeli, kasema, "Daudi, fanya yote yaliyo ndani ya moyo wako, kwa maana Mungu yu pamoja nawe. Wewe ni chombo cha Mungu kilichotiwa mafuta."

224 Lakini huyo akiwa ni nabii, na kosa lake, na Mungu anawajibika kwa nabii Wake. Usiku huo Yeye alimtokea, akasema, "Enenda, ukamwambie mtumishi wangu Daudi, ninapenda ujasiri wake, ninampenda kwa ajili ya jambo hili, maana yeye ni mtu anayeupendeza moyo Wangu, na ninajua wakati umewadia kwa sanduku langu kuwa hivyo, kuwekwa chini na kitu fulani, lakini mimi ninaninii tu. . . Hayo si majira

ya jambo hilo kutukia. Nitamwachia mwanawe afanye jambo hilo, lakini Mimi sitamruhusu afanye jambo hilo.”

225 Ndipo huyu hapa Nathani anakuja akiwa na, “BWANA ASEMA HIVI, Daudi, huo ufunuo mkubwa uliokuwa nao ni wa uongo kama ulivyokuwa wakati ulipolipandisha sanduku.” (A-ha! A-ha! Unaona?) “Usifanye jambo hilo! Usijaribu! Lakini Mungu alisema atamtumia ‘mwanao atimize hilo.’” Hapo! Unaona? Haya basi!

226 Daudi alikuwa ametiwa mafuta kusema hayo kwa sababu angeweza kuona jambo hilo hapo awali, kama tu vile Ibrahimu alivyoutafuta Mji hapa duniani. Unajua, alikuwa akiutafuta kwa sababu yeye alikuwa yuaenda kuishi hapa siku moja, Ibrahimu ataishi hapa, katika Mji huo. Basi alizunguka akiutafuta. Na mahali pale pale alipoutafuta, ulikuwa tu juu yake wakati huo, nao utarudi katika ule Utawala wa Miaka Elfu naye ataishi katika Mji huo. Lakini yeye akiwa ni nabii, alikuwa amechaguliwa na kuvuviwa, alijua kulikuwako na Mji fulani mahali fulani, naye alikuwa akiutafuta. Lakini, unaona, yeye alifichwa ufunuo wote wa jambo hilo, haukuwa kwa ajili ya wakati wake . . . na kuendelea hata kwa Yohana, ambapo aliuona ukishuka kutoka Mbinguni kwa Mungu. Mji huo ulikuwa ndio huo.

227 Unaona, kila kitu hakina budi kuwa katika majira yake. Unapanda ngano yako katika majira ya kuchipusha na . . . ama kwenye majira ya kupukutika majani na kuivuna majira yajayo ya kiangazi. Unaona? Haina budi kuja kupitia kwenye ubua, halafu kuja kupitia kwenye kishada, na kapi, na kuendelea hadi kwenye . . . Haina budi kuwa katika wakati wake. Maumbile yote yanaenda katika uhusiano. Roho wa Mungu aliumba maumbile, na yote ya Mungu na maumbile Yake yako katika uhusiano. Vitu hivi vyote vilivyowekwa hekaluni vilikuwa ni kioleza cha yale aliyoona Mbinguni.

228 Ukiona mti ukikazana kung’ang’ania kuishi, hiyo ina maana kwamba kuna mti usiokufa. Ukimwona mtu akipigania kuishi, inaonyesha ya kwamba kuna maskani inayongoja mahali fulani isiyokufa. ”Kama nyumba ya maskani yetu iliyo ya dunia hii ikiharibiwa; tuna moja inayongoja.” Baba mwema wa Mbinguni aliniruhusu kutembea nyuma ya pazia hilo siku moja na kuiona. Ni wangapi waliosikia hadithi hiyo . . . ? . . . Unaona? Kuangalia ng’ambo ya pazia la wakati. Ilikuwa kule sawasawa na hivi ninavyowahubiri ninyi nyote, walikuwa hapo wamesimama. Nafsi zilizo chini ya madhabahu zikilia, “Hata lini?” Si hadithi tu ya kubuniwa, mtu fulani aliyekuwa na akili: “Hata lini, Bwana?” Unaona? Wakati tukihisi hayo hivi sasa, kama wakati wetu, kama Ndugu Bill Dauch anayeketi hapa mwenye umri wa miaka tisini na mitatu. Kuna kitu fulani kinachomtamani huyo kijana mwanamume, tena. Kuna kitu fulani . . . Ungetoa cho chote. Jinsi ningependa jambo hilo. Ndugu Jack, na sisi wengine

wote. Kurudi, Ndugu Gerholtzer, hapa ndani, tuingie katika huo ujana. Unataka kufanya jambo hilo kwa ajili gani? Kuwa kijana na kuzurura huku na huko? La, bwana! Ni kwa sababu tunajisikia tungepata wakati zaidi wa kumtukuza Mungu huyu tunayempenda.

229 Na ndugu zangu wapendwa, nina Ujumbe huu asubuhi ya leo, kuna Nchi iliyo ng'ambo ya mto wanayaoiita hiyo tamu milele. Huko tutamtukuza Yeye daima, na nyakati zote, na Milele. Ni kwa nini tunasikia jambo hilo? Ni kwa sababu kilindi kinaita kilindi. Na mradi tu kilindi kinaita, hapana budi pawe na kilindi kinachojibu mwito huo la sivyo hakungekuwako na mwito wo wote. Kabla hapajakuwapo na kiumbe, hapana budi pawe na muumba kwanza wa kuumba kiumbe hicho, la sivyo hapana . . . Hiyo inaonyesha ushahidi wa kweli kwamba yuko.

230 Angalia makasisi hawa, wote wako nje ya mstari. Angalia ule upako, vema, ule upako hauna shida yo yote. Vivyo hivyo na kwenu ninyi Wapentekoste, lakini angalia unaingia kwenye njia gani ya mawasiliano sasa. Siku zimebadilika tangu Pentekoste, kuna jambo jingine kwa ajili yetu. Kama kusingekuwako na nabii nchini, labda Daudi angalikuwa sahihi. Hiyo ni kweli. Lakini Nathani alisimama hapo, mtu aliyethibitishwa, aliyechaguliwa, akashuhudiwa na Mungu kwamba ni nabii.

231 Angalia! Lile sanduku katika Biblia daima ni mfano wa Neno kwetu, kwa sababu lililokuwa ndani ya sanduku ni Neno la Mungu. Na lilikuwa . . . Angalia sanduku walilolileta, angalia vile walivyofanya jambo hilo. Halikuwa limewekwa mahali pa asili palipochaguliwa na Mungu. Sasa, Mungu alisema nyuma hapa katika Torati ya kwamba halina budi . . . jinsi linavyopaswa kufanyika, jinsi sanduku hili linavyopaswa kubebwa, na kwamba libebwe na nani. Lakini Daudi, chini ya upako wake . . .

232 Ndugu zangu, msikose jambo hili. Nanyi dada zangu, ninyi mnaotaka kuwa wahubiri wanawake na kadhalika, msikose jambo hili. Haidhuru una upako wa namna gani, huna budi kuingia mahali palipoandaliwa na Mungu. Upako wa Daudi ulikuwa ni sawa, lakini katika kufanya jambo hilo yeye alishikwa na hisia kali na akaruka mpaka. Yeye alifanya nini? Aliruka mpaka. Badala ya kuliweka lile sanduku mahali pake pa asili, alilibeba juu ya gari jipya na wala si juu ya mioyo ya Walawi. Lilipaswa kubebwa juu ya mabega ya Walawi, ambapo ni juu ya moyo. Neno haliko akilini, liko moyoni! "Si juu ya gari jipya." Hiyo ilikuwa ni nini? Baadhi . . . Iliwakilisha kitu kipya, Daudi alichofanya pale, alinena habari za kila madhehebu ambayo yatakayotokea. Neno la Mungu halipaswi kuninii kwa . . . kubebwa na wazee wa jimbo ama maaskofu, na kadhalika, wa madhehebu. Ni ubatizo wa Roho Mtakatifu katika moyo wa mwanadamu, wala si katika mwenendo fulani

wa kikanisa. Roho Mtakatifu ni hazina ya upendo wa Mungu katika moyo wa mwanamume na wanawake kutii. Unaona?

233 Lilikuwa juu ya mabega ya wahudumu Wake, wahudumu Wake walikuwa ni Walawi. Waliliweka juu ya bega lao la kushoto na kubeba hilo sanduku namna hiyo, kwa sababu lilikuwa juu ya moyo wao. Walikuwa na mzigo wa Neno moyoni mwao. Amina! Sasa una mzigo wa madhehebu yako juu ya moyo wako, mzigo wa kusanyiko lako: kama utajenga *hili*, ama kufanya *vile*, ama kufanya jambo lingine. Mzigo wa kwamba utawaingiza wangapi zaidi katika madhehebu yako; badala ya mzigo wa Neno la Bwana, mpaka watu wataona Neno la Mungu peke yake wala si kitu kingine. Lakini mmeliweka juu ya gari jipya sasa. Unaona? Hata wanalibemba hapa kwenye baraza la ekumeni, kwenye mabega. Mimi sitaki kukosoa, naomba Mungu anisaidie. Ninawaambieni tu Kweli.

234 Sasa, huku wao wakiwa wameshawishiwa na kanuni za imani na mabaraza ya ekumeni, Neno, Neno halisi la majira hayo lilipuuzwa, kwa sababu walikuwa na mhemuko mwingi sana. Lakini Daudi, mfalme aliyetiwa mafuta . . . Yeye alikuwa ni mfalme, lakini alitiwa mafuta kama *mfalme*. Unasema, "Mimi ni mhudumu, nimetiwa mafuta." Basi dumu kuwa mhudumu, usijaribu kuwa nabii. Unaona? Kama wewe ni mwijilisti, dumu kuwa mwijilisti.

235 Kumbukeni Uzia, katika siku za Isaya, yule mfalme kijana . . . yule nabii kijana. Uzia alikuwa ni mtu mkuu, mtu aliyetiwa mafuta, Mungu alimbariki; alijibariki mwenyewe. Naam, niliwahubirieni juu ya jambo hilo hapa wakati mmoja. Basi siku moja alijiinua sana hata akafikiri angeweza kuchukua ofisi ya kuhani, ndipo akachukua ninii . . . hatimaye akaenda mbele za Bwana, na ninii . . . hao makuhani wakamwambia, "Usifanye jambo hilo, Uzia!" Lakini akajitukuza. Nabii hangeweza kumwambia jambo lo lote. Makuhani walijua utaratibu wao, walikuwa wakidumisha ukuhani wao, akasema, "Hilo si agizo lako, Uzia, Usifanye jambo hilo!"

236 Vema, yeye aliwafanya "Funga mdomo!" Naye akaenda na—akaenda na ule moto, akaingia akatoe sadaka, kuchukua kazi ya kuhani; alikuwa ametiwa mafuta kama mfalme, wala si kuhani. Na hao makuhani walikuwa wakijaribu kumwambia, "Wewe ni mfalme mzuri sana, umetiwa mafuta, Mungu ametubariki sasa; lakini wewe ni mfalme, wala si kuhani."

237 Nanyi wachungaji kamwe hampaswi kumwambia nabii la kufanya, wala ninyi wainjilisti kumwambia mchungaji. Unaona, kila mmoja ana ofisi yake kama imetambulishwa kikamilifu.

238 Kwa hiyo akaingia na ule moto, ndipo akapigwa kwa ukoma akafa.

239 Sasa huyu hapa Daudi, mfalme, Daudi anajaribu kufanya jambo lile lile hapa. Amejichukulia hilo mwenyewe. "Vema, hilo

ni sawa, sina budi kwenda. Angalia, watu wengi. Unasema nini, jemadari? Ati una elfu kumi."

240 "Mungu na atukuzwe, Daudi, namsihi Roho." Loo, alimsihi! Kweli alimsihi. "Unafikiri nini, Daudi? Unamsihi?"

241 "Mungu na atukukuzwe, yuko kila mahali mwilini mwangu! Hebu na tulichunguze tuone kama ni kweli, hebu tuone. Sanduku ni la wapi?"

242 "Ni la kwetu! Ni mali yetu."

243 "Ni nani tunayepaswa kumtaka shauri? Hakika, sanduku. Ni sawasawa tu na vile ile ardhi ilivyokuwa ni—ni ya Israeli badala ya Wafilisti. Hiyo ni kweli. Ni vyetu. Na ni kama vile ninavyosikia upako, pia."

244 Maakida wa mamia, kusanyiko lote, "Mungu atukuzwe!" Wakapiga makofi, na wakapiga makelele, na wakacheza, na kurukaruka.

245 Wao walikuwa na Roho, lakini unafikiri Baba alikuwa akiwazia jambo gani? "Jinsi nilivyomtuma Nathani, yule nabii kule chini! Wao wanajua la kufanya, na vivyo hivyo Daudi, lakini sasa yeye ana shauku sana na amevuka mpaka wake moja kwa moja na akaenda kufanya jambo *hili*."

246 Vema, angalia, "libebeni mabegani" ulikuwa ndio mpango wa kwanza wa Mungu. Kuna *lazima* tano. Ninawatakeni mwandike hizi, kama mnaninii . . . ninawaona mnaandika. (Na ni dakika ishirini, saa nne na dakika ishirini na kitu, kwa hiyo nitajaribu kumaliza kwenye saa tano; Nitaharakisha upesi niwezavyo.) Haidhuru mtu anamfanyia Mungu kazi kwa uaminifu jinsi gani, haidhuru ni mwaminifu jinsi gani, ametiwa mafuta kiasi gani, ni Mpresbiteri namna gani, Mbatisti, Mpentekoste; haidhuru kama wewe ni askofu, shemasi, hata uwe nani, mchungaji, mwinjilisti, nabii, ye yote uwezaye kuwa; kuna lazima tano ambazo hazina budi kufikiriwa kwanza. Haidhuru ni kiasi gani cha upako, jinsi linavyoonekana ni zuri, jinsi watu wanavyopiga makelele, kila kitu anachofanya Roho, kuna *lazima*.

247 Sasa, ndugu zangu, wakati mnapotayarisha makaratasi yenu, je! mnaweza kuelewa sasa ni kwa nini? Sasa kumbukeni, ninyi nyote mmefikiria, na imefundishwa kati yenu, si . . . (unaona, ninazungumza kote nchini) . . . ya kwamba sikuamini katika kunena kwa lugha. Ninaamini katika kunena kwa lugha, lakini ungali unaweza kunena kwa lugha wala usiwe na Roho Mtakatifu. I Wakorintho 13, inasema, "Nijaposema kwa lugha za binadamu na za malaika, mimi si kitu bado." Unaona? Huo ni upako wa Roho Mtakatifu, huo hauna uhusiano wo wote na nafsi iliyo ndani yako. Unaweza kunena kwa lugha na kukana Neno. Nimeona hilo likitendeka, nanyi mnaliona hilo pia. Unaona? Mwanamke anaweza kuhubiri Injili na . . . Unaona? Wanaweza kufanya yote . . . Wanakata nywele zao, na bado wapige makelele

na kunena kwa lugha na cho chote kile. A-ha, hiyo ni kweli kabisa. Huna budi kuchukuana na Kweli ya Neno.

248 Angalia! Haidhuru mtu ni mwaminifu jinsi gani, haidhuru anatumiwa na Mungu jinsi gani, haidhuru yeye ni nani, hana budi kuwa hivi: hana budi . . . Jambo analonena habari zake halina budi kuwa katika wakati unaofaa wa Biblia. Mtu fulani anasema, "Vema, Musa kule nyuma." Ninajua Musa alilofanya, lakini hivyo sivyo Mungu anavyofanya siku hizi. "Vema, kule nyuma, miaka thelathini iliyopita, Luther alisema . . . " Huenda hilo likawa ni sawa, lakini hivyo sivyo anavyofanya siku hizi. "Vema, miaka arobaini iliyopita, Pentekoste ilishuka." Lakini hicho sicho anachofanya siku hizi. Unaona? Halina budi kuwa katika wakati wake.

249 Halina budi kuwa ni kulingana na Maandiko. Halina budi kuwa ni katika wakati wake, la pili. La tatu, halina budi kuwa ni sawasawa na vile Neno la Mungu lilivyosema litakuwa.

250 Nawe unasema, "Mungu atukuzwe! Roho Mtakatifu alishuka juu yangu, haleluya, kama tu vile alivyofanya kwenye siku ya Pentekoste." Lakini hilo linaweza liwe ni tofauti siku hizi. Alishuka juu ya Daudi, pia, sivyo? Hakika, alishuka. Alishuka juu ya Uzia, lakini ilikuwa ni makosa! Unaona, huna budi kuingia kwenye kilindi zaidi ya hapo. Unaona? Huna budi kuingia kwenye kilindi zaidi ya hapo. Sasa, msiudhike, iweni tu—tu na kicho. Unaona?

251 Pia angalia, na pia halina budi kuja kwa mtu aliyechaguliwa na Mungu. Si mwenye kuchaguliwa na madhehebu, si wa kuchaguliwa na watu, lakini kulingana na uchaguzi wa Mungu. Na kama ni Ujumbe kutoka kwa Mungu, wa ufunuo mkuu kutoka kwa Mungu, hauna budi kuja kwa nabii Wake. Sasa, kama unataka Maandiko ya jambo hilo, ni Amosi 3:7. Unaona? Sasa, haina budi kuwa.

252 Kuna mambo matano halina budi kuwa: halina budi kuwa katika wakati wake. Halina budi kuwa kwenye wakati ambao Mungu alisema litakuwa. Halina budi kuwa limeandikwa katika Neno la Mungu. Halina budi kuwa katika majira ya wakati wa Mungu, unaona. Na halina budi kuwa ni kwa uchaguzi wa Mungu.

253 Na Mungu hahitaji ye yote wetu kufasiri Neno Lake, Mungu hujifasiria Mwenyewe. Hahitaji seminari zetu. Hahitaji hekima yetu, ni upuuzi. Unaona? Hawa alipata hiyo, a-ha, na akakosa ile Tafsiri kwa hekima yake.

254 Unasema, "Loo, jamani, jamaa huyo ni mtu mwenye akili." Vema, hilo halimaanishi kitu. Hakika. Ahabu alikuwa mtu mwerevu. Belteshaza alikuwa ni mtu mwerevu. Shetani alikuwa ni mjanja, mjuvi, na mwerevu kuliko wote, hakuna mtu angaliweza kumshinda, hakuna kabisa.

255 Sitegemei . . . hakuna . . . hakuna hekima, ninamtegemea Mungu tu. Unaona? Mungu yukoje? Yeye ni Neno. Na basi Mungu anatafsirije Neno Lake Mwenyewe? Sikiliza kwa makini sasa, usiyakose mambo haya. Mungu anatafsirije Neno Lake Mwenyewe? Kwa kulifanya litimie, si tu *moja* hapa, lakini ni *lote* kwa ajili ya majira hayo.

256 Si kusema, "Nuhu toka uende ukahubiri," mwenye uvuvio, lakini, "Jenga safina, iwekee milango, uijenge *hivi*, na *vile*." Vipi kama alingeweka mlango juu badala ya chini? Vipi kama angaliweka dirisha chini, mlango juu? Unaona? Haina budi kuelekezwa kulingana na wakati, kwa sababu hivyo ndivyo hasa Mungu atakavyoitumia. Haina budi kuwa namna hiyo, na haina budi kuja kwa uvuvio.

257 Nilisikia jamaa fulani akisema siku moja, kasema, "Ninaamini mtu huyo anawaombea wagonjwa, ninaamini ni jambo zuri sana. Lakini kuhusu yeye kuwa nabii," kasema "Ninaamini yeye ni nabii wa Mungu; lakini kama mwalimu, mbona, yeye ni wa 'Yesu pekee.'" Ungeweza . . . Ungemwita huyo ni mtu wa aina gani? Mtu asiyejua analozungumzia.

258 Neno lenyewe *nabii* linamaanisha kwamba "Yeye ni mfunuzi wa Neno la Mungu," fasiri huja tu kwa huyo. Na hiyo ndiyo sababu siku hizi tuna haja sana na mtu huyu mkuu ambaye anapaswa kutumwa kwetu katika namna ya nabii Eliya, kwa sababu itakuwa ni ufunuo wa Mungu ukijulishwa kwetu kwa kuthibitishwa, ikionyesha ya kwamba ni siku na saa na majira ambayo Mungu aliahidi jambo hilo litakuwa. Na, kumbukeni, atanenwa vibaya; imekuwa hivyo daima, itakuwa hivyo daima. Amekataliwa, kama tu vile gugu litakavyoondoka . . . Kwanza atakubaliwa, kwa sababu gugu hushikilia ngano tu mpaka itakapoweza kulifikia jua. Pentekoste itausetiri tu Ujumbe, kuupa mlango uliofunguliwa mpaka utakaposambazwa, ndipo gugu litakapoondoka, nayo ngano itakaa katika Uwepo wa Mwana, unaona, ipate kuiva.

259 Hakutakuwako na madhehebu yo yote, kumbukeni tu. Ndugu Jack hapa ni mwanahistoria, wengi wenu ninyi watu hapa ni wanahistoria. Hapajawahi kuwa na ufufuo ila yapata mika mitatu baada ya huo ufufuo wao wakaanza madhehebu kwake. Hiyo ni kweli? Na muujiza huu mkuu wa mwisho wa mwenendo wa Mungu katika siku hizi za mwisho, umeendelea miaka ishirini; na uko maili milioni moja kutoka kwa madhehebu, daima unazidi kwenda mbali; kapi linajiondoa, hakuna ushirikiano, hakuna uhusiano wo wote Nalo. Unaona? Daima linajiondoa Kwake. Hakuwezi kuweko na mengine, ni ngano sasa. Lakini sisi ni wabichi sana, a-ha. Hiyo ni kweli. Inatupasa kukaa katika Uwepo wa Mwana tupate kuivishwa, hivyo tu. Wabichi sana; hatuna unyofu, utakatifu, jambo ambalo tunalopaswa kuwa nalo kati yetu, kujua ya kwamba Roho

wa Mungu aliye hai, akitenda kazi katika Neno Lake na badoanatuonyesha mambo.

260 Tuna waigaji wa uongo wanaoinuka. Hao ni kwa ajili gani? Kudanganya. Biblia ilisema watadanganya. "Kama Yambre na Yane walivyopingana na Musa, vivyo hivyo na hawa katika siku za mwisho." Unaona? Wanafanya jambo lile lile, wanakuja moja kwa moja wakiigiza Hilo, ni vile vile kabisa. Unaona? Iweni waangalifu! Angalieni fundisho la Biblia. Angalieni ujumbe unaofuata hizo ishara! Ingali ni itikadi ile ile ya kale ya ujumbe? Sahau!

261 Mungu alituma miujiza na ishara kuvuta usikivu wa watu Wake. Wakati Yesu alipokuja akiwa tu anaponya wagonjwa na kadhalika, vivyo hivyo na manabii. Wao walifikiri, "Loo, utukufu, Yeye yuaja, atakuwa Mfarisayo. Atakuwa Msadukayo."

262 Lakini, Yeye alisema, "Enyi uzao wa nyoka na majoka." Kasema, "Ninyi ni wa baba yenu Ibilisi, kazi zake mtazifanya." Kasema, "Msipoula mwili wake Mwana wa Adamu, na kuinywa Damu Yake, hakuna Uzima ndani yenu." Yeye hakuelezea jambo Hilo. Haikumbidi kulielezea. Haleluya. Hilo lilikuwa ni kwa ajili ya majira mengine. A-ha. Alisema tu yale aliyopaswa kusema, "Mimi daima ninafanya yale yanayompendeza Baba, na hiyo ni kutii Neno Lake. Kama silitii, maisha Yangu na kazi Zangu havilingani na Neno Lake ninalopaswa kufanya, basi msiniamini, Mimi si Yeye; lakini kama vinalingana, basi aminini hizo kazi kama hamwezi kuniamini Mimi," akasema.

263 Angalia sasa hizi *lazima* ambazo hazina budi kufanywa.

264 Sasa, ona, Mungu hakuwa amewafunulia jambo hilo kwa njia Yake aliyoiandaa, alikuwa ameifunua kwa uvuvio, lakini ilikuwa ni kwa njia mbaya. Unaona, uvuvio utakuwa ni sawa, lakini kama uko kwenye njia mbaya, utapelekwa vibaya. Kama vile ukichukua risasi na kuilenga moja kwa moja kwenye shabaha, inaelekea moja kwa moja kwenye shabaha, lakini mpulizio wa upepo unaweza kuipindisha vibaya. Sasa, katika motokaa yako, ukiendesha barabarani kwa maili sitini, sabini kwa saa na mpulizio wa upepo unakupulizia, unaweza kunyosha magurudumu yako, uyarudishe barabarani tena. Lakini risasi huwezi; hakuna kitu hapo cha kunyosha magurudumu yake, itakosa shabaha. Unaona, haina budi kwenda kwenye njia yake ya asili.

265 Vivyo hivyo na Neno la Mungu halina budi kwenda katika njia Yake ya asili. Hakuna mpulizio mdogo wa upepo utakaoliondoa, hakuna madhehebu madogo yatakayoliondoa, hakuna mateso madogo yatakayoliondoa, limeelekezwa kwenye shabaha! Litapiga pale, pia. Halafu Mungu . . . Wakati litakapopiga sehemu hiyo, Mungu atalithibitisha, "Katikati kabisa!" A-ha, ni vile vile hasa alivyosema atafanya. Hili hapa

katika Maandiko, hii, “BWANA ASEMA HIVI, ‘litatimia!’” Hii hapa. Unaona? Haya basi.

266 Sasa, Mungu hakuwa amelifunua kwa njia Yake iliyoandaliwa. Kwa hiyo wakaanza kulifanya bila ya Neno Lake, na nje ya majira yake, vile vile tu wamefanya leo. Wakati mwanadamu, hata awe mwaminifu namna gani, anapojaribu kumtendea kazi nje ya njia Yake iliyoandaliwa, sikuzote wanaivuruga. Kama vile Balaamu, Balaamu alifikiri alikuwa akimtendea Mungu kazi.

267 Unafikiri Mungu husema uongo? Je! Mungu wakati wo wote hubadilisha nia Yake? Vema, watu wanatenda siku hizi kama alivyofanya Yeye. Wakati aliposema wanawake wasikate nywele zao; wao wanasema, “Tunaweza kuzikata, Dk. *Fulani* alisema tunaweza. Ndugu *Fulani* alisema ya kwamba wewe ni kwamba tu una mawazo finyu sana.” A-ha, a-ha. Unaona?

268 “Vema, jambo *hili* linaweza kutukia? *Hili* linaweza kutukia?”

269 “Naam, a-ha, *Fulani* alisema hivyo.”

270 Mungu habadilishi nia yake.

271 Je! unaamini ya kwamba Balaamu alikuwa ni nabii? Biblia ilisema alikuwa. Unaamini alikuwa nabii? Sasa, kumbuka, Balaki alimjia na kusema, “Shuka uende ukawalaani watu hawa, kwa maana wamejaa katika uso wa dunia. Wao hata si madhehebu, si taifa, ni kundi tu lililotawanyika tu; nasi ndio watu mashuhuri wa nchi. Sasa wewe shuka uende kule ukawalaani hao watu, nami nitakulipa kwa ajili ya jambo hilo.”

272 Na Balaamu alifanya vile hasa nabii anavyopaswa kufanya, akasema, “Sitaenda. Ninyi ngojeni tu hapa kwa usiku kucha, hebu nione Mungu atasema nifanye nini.”

273 Kwa hiyo akaingia, akasema, “Bwana, kuna watu hapa nje pamoja nami ambao wamekuja, walinitaka nishuke niende nikawalaani watu wengine huko chini.” Kasema, “Unataka nifanye nini juu ya jambo hilo?”

274 Mungu akasema, “Usiende, kwa kuwa hao ni watu Wangu!”

275 Balaamu akatoka akaenda, kasema, “Rudini nyumbani kwenu. Siwezi kuambatana nanyi, Mungu aliniambia nisifanye jambo hilo.” Sasa, hilo hapo Neno la Mungu la asili: “Usiende!”

276 Vema, ndipo wakarudi, kasema, “Unajua, askofu wako hangesikiliza.”

277 “Vema,” mfalme akasema, “nitakwambia tutakalofanya. Yeye anahitaji pesa kidogo, ninaamini ya kwamba hizo zinaweza kumshawishi. Ama labda nitamfanya mzee wa jimbo, labda nitampa kitu fulani kikubwa cha kufanya. Huenda nikamfanya askofu, huwezi kujua jambo ninaloweza kufanya. Hapa, nitawaambia nitakalofanya. Ninyi watu hamna elimu

ya kutosha ya kumshawishi hata hivyo; *yake, yenu*, na *akuna*, na *chumla*, na *pepa* na *jukua*, si sahihi. Yeye hatawasikiliza, tutatuma kundi lenye elimu kweli kweli kule, watu wengine zaidi mashuhuri."

278 Wakashuka wakaenda kule chini, kasema, "Datari Balaamu, *Daktari* Balaamu, salamu. Ninakuletea salamu kutoka kwa mfalme."

279 "Subalkheri, ndugu zangu." Unaona?

280 "Sasa, Daktari Balaamu . . . " Na, loo, msamiati huo, jinsi ulivyomwagwa kweli kweli. Kisha kasema, "Sasa, mfalme amesema ya kwamba atakupandisha cheo, pia atakupa heshima kubwa. Na, unajua, walikupa kiasi *fulani* tu cha pesa kuchukua jukumu hili, lakini mfalme anasema atakizidisha mara tatu, mara nne, kama ukija tu kuzichukua." Ndipo, Balaamu, akaingiwa na hamu ya kupata faida ya haraka. Akapata mawazo ya kijinga na akachochea akili zake.

281 Sasa, kumbuka, yeye alimwita Mungu kwa huo, upako uliotiwa, lakini alimsukuma Mungu moja kwa moja kutoka kwenye mpango wa asili. Na hivyo ndivyo Wapentekoste walivyofanya hasa! Kupendwa na watu wengi, ninyi wa Umoja, ninyi wa Utatu, kusudi mpendwe na watu wengi mliunda madhehebu mpate kuwa tofauti, mliunda madhehebu na mmekufa! Kamwe hamtainuka tena. Lakini, unaona, mlipaswa kudumu na Neno la Mungu la asi- . . . Yeye aliwavuta akawatoa kutoka hiyo Assembly kuwafanya watu, lakini mliunda madhehebu na kurudi moja kwa moja kwenye matapiko yale yale (samahani) mliyotoka kwake, takataka zile zile mlizotoka kwake "Kama mbwa anavyoenda kwenye matapiko yake na nguruwe kugaagaa matopeni mwake." Samahani nilisema jambo hilo, samahani, hilo si jambo zuri kwa jukwaa hili hapa. Mnaona? Nilisema jambo hilo tu katika mwili. Angalia sasa ya kwamba hilo ndilo ninalomaanisha, matapiko. Ningepaswa kusema hivyo. Neno lenyewe lilikuwa ni sawa, lakini lilitumiwa tu vibaya. Unaona? Lilitumiwa vizuri, lakini likasikika tu vibaya, a-ha . . .? . . . Matapiko, "Kama mbwa anavyoyarudia matapiko yake."

282 Kama Assemblies of God, Baraza Kuu, lilivyofanya Pentekoste kuwa madhehebu mwanzoni na kuwaingiza katika jambo hilo hivi kwamba hawangeweza kukubali ufunuo, je! hamjui, Waumoja, mlifanya jambo lile lile. Mngewezaje kupokea ujumbe wa *uzao wa nyoka*, *Usalama wa milele*, na mambo haya mengine ambayo yametokea? Ninyi mmejifunga kweli kweli kwa madhehebu hata hamtaukubali Huo kwenye mlango wenu, a-ha, a-ha, jambo lile lile alilofanya Balaamu. Lakini Mungu hakubadilisha nia Yake.

283 Kwa hiyo Balaamu akaenda kule na kusema, "Bwana, sasa angalia, nina nafasi kweli leo kuwa mtu mashuhuri.

Unajua nilikuwa mtu duni, lakini nina nafasi ya kuwa mtu mashuhuri. Unasemaje sasa juu yake, Bwana?" Sasa, hangepaswa kamwe kusema jambo hilo! Alijua sawasawa hasa vile Mungu alivyosema afanye!

284 Vivyo hivyo na kila mmoja wenu ambaye amebatizwa katika Jina la "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu," juu ya masuala haya mengine yote ya Biblia yanayopaswa kuwa katika siku hii, mnajua la kufanya kuhusu Hilo, ni kuukubali Huo! Mnapomwona Mungu akithibitisha dhahiri "Ni Kweli," huyo ni Mungu akifasiri Neno Lake Mwenyewe. Lakini je! mtafanya jambo hilo? La, madhehebu yenu hayatawaruhusu kufanya jambo hilo!

285 Wengi wa wahudumu kule Tucson ambao wanasikiliza asubuhi ya leo, Ndugu Gilmore, sina kitu dhidi yenu; Ndugu Brock, Assembly ya Kwanza, na kanisa la Friendly. Ninyi watu, nilikuwa huko wakati huo wote, hata hamkuniruhusu kuingia. Mimi. . .Hakika, hamngeweza, hamwezi na mbaki jinsi mlivyo. Hamwezi kukubali ufunuo, maana mmeunda madhehebu. Basi sikilizeni, kama tu vile Uzia alivyouawa kwa sababu alikuwa chini ya uvuvio huo wa uongo, vivyo hivyo na Wakristo wengi wa kweli wanapoteza ujuzi wao kule nyuma katika madhehebu hayo ya kale yaliyokufa, kwa sababu wanaweka mkono wao kwenye Sanduku wakati hawajachaguliwa kufanya hivyo. Sasa mnaweza kuamini jambo Hilo, ama kutokuamini jambo Hilo, hiyo ni juu yenu. Mungu ndiye Hakimu wenu. Mungu kamwe hajapata kughairi Neno Lake. Yale aliyosema mara ya kwanza, yeye anayasema kwa kila wakati.

286 Halafu Balaamu, "Usiende!"

287 Ndipo Balaamu akarudi, kasema, "Lakini Bwana, je! niende?"

288 Sasa angalia! Mungu alisema, "Nenda!" Sasa, alimpa ruhusa ya kwenda. Kuna mapenzi ya kuruhusia ya Mungu, wala si mapenzi asili ya Mungu. Unaona jinsi alivyoingia katika shida?

289 Na mtu ye yote anayejenga cho chote, madhehebu yo yote, ama cho chote nje ya Neno la Mungu, ni changarawe inayotikisika nacho kitaanguka! Hakika kitakufa kama kitu kingine, kwa maana Neno la Mungu ni Mwili wa Bibi-arusi unaokua. Huwezi kuufanya wote kuwa ni mguu, wote ni mkono, wote ni paja. Mambo haya yanakuja katika majira yake.

290 Na Pentekoste, mlilifanya lote kitu kimoja, kwa hiyo hamwezi kukubali ufunuo mpya. Hiyo ndiyo sababu mnakaa mahali papo hapo mlipo na kufa; linasonga mbele. (Mengi sana, nitawachosha.) Lakini Mungu habadilishi nia Yake, uamuzi Wake wa kwanza ni sahihi kabisa. Kwa hiyo Mungu habadilishi nia Yake, anakuacha tu uendelee katika mapenzi yako ya kuruhusia. "Mungu ni Mungu mwema," kama Oral Roberts anavyosema. Yeye pia ni Mungu wa kuogofya!

291 Angalia, ni kama tu mnavyosema, "Mungu atukuzwe, ninataka kunena kwa lugha!" Atakuacha ufanye hivyo, lakini hiyo si ishara ya kwamba una Roho Mtakatifu.

292 Mnambuka vile Tomaso alivyosema, yule mwenye mashaka wa kale? "Isipokuwa niwe na ushahidi, sina budi kutia vidole vyangu katika misumari Yake, mikono Yake, na ubavuni Mwake, si—si—si—sitaamini." Sasa, hivyo ndivyo iliyo, jambo lile lile.

293 Yesu alisema, "Haya basi, Tomaso, ingiza mikono yako hapa ndani basi kama hivyo ndivyo unavyotaka kujua." Unaona? Unaona? Sasa, kama wewe ni Tomaso, basi, endelea. Lakini yeye alisema nini? "Ni zaidi sana vipi thawabu yao wale wasioona bali wanasadiki." A-ha.

294 Angalia, angalia, kwa kufanya jambo hili, yeye alisababisha kifo cha mtu mwenye moyo safi; kuweka mkono wake kwenye Sanduku wakati hakupaswa kufanya, hivyo. Mtu mashuhuri, mwaminifu, alifikiri ule upako na kila kitu vilikuwa ni sawa, lakini sanduku lilikuwa likienda upande mbaya. "Ng'ombe," Biblia ilisema, "alijikunguwaa," si Walawi. Maksai alijikunguwaa na gari lilikuwa likipinduka; na mtu mwaminifu, moyo wake umejaa upendo, akaweka mkono wake kwenye sanduku hilo apate kulishikilia lisianguke, naye akapigwa akafa kwa sababu hakuna mtu angaliweza kugusa sanduku hilo ila Mlawi. Unaona jinsi Mungu anavyoshikilia Neno Lake, jinsi anavyodumu na njia Yake, jinsi anavyoweka utaratibu Wake? Uzia alipigwa kwa ukoma. Huyu hapa Daudi, kwa jumla alisababisha kifo cha mtu, na msiba mkubwa; akiwa ametiwa mafuta na Roho, wote wawili, lakini akiwa yuko nje ya njia ya Mungu. Hiyo ni kweli? Akafa. Loo, lilimwogopesha Daudi hata kufa, akaita ji—jina la mahali hapo, kama vile Ndugu Jack alivyolisoma. Unaona? Alimtia alama pale.

295 Ni mara ngapi madhehebu yamefanya jambo lile lile kwa waamini wanyofu. Kanisa Katoliki, Methodisti, Batisti, Kanisa la Kristo, hata Wapentekoste, wamesababisha vifo vingi vya kiroho kwa jambo lile lile. Wakati yalipokuja, na mambo haya, waliona . . . wala hawawezi kuendelea mbele zaidi, kwa sababu hivyo ndivyo madhehebu yao yanavyoamini.

296 Angalia siku hizi, ile mikutano mikubwa, jambo lile lile. Hawafanyi kitu ila kuwafanya "watoto wa kuzimu maradufu, wabaya kuliko walivyokuwa kwanza." Wanawafanya wagumu zaidi, kwa kweli, kuja kwenye ile Kweli. Wanakuwa na mmoja wa huu ufufuo mkubwa, na wote wanaingia, wanaendelea kwa kitambo kidogo, kisha wanarudi na kuanza dhambi hii yote tena. Wanasikia juu ya ufufuo mwingine, wanasema, "Ala, nilikuwa na upuuzi mwingi sana; niliujaribu, ni bure." Unaona? Hawaijui ile njia. Hawaoni.

297 Nilimsikia mwijilisti wetu mkuu Billy Graham, aliketi asubuhi moja kwenye kiamshakinywa kama hiki, ndipo

akasema, "Mimi..." Hapa, anainua Biblia, kule Louisville, Kentucky, kasema, "*Huo hapo* mfano wa Mungu." Na hiyo ni kweli, mtu huyo alisema kweli. Alisema, "Unaenda... Paulo aliingia katika mji mmoja na akapata mwongofu mmoja, akarudi mwaka mmoja baadaye akakuta thelathini kutokana na huyo mwongofu." Kasema, "Lakini ninaingia katika mji mmoja na kuwapata waongofu elfu thelathini, kisha ninarudi miezi sita baadaye wala siwezi kupata thelathini." Akasema, "Mnajua kuna nini?" Kasema, "Enyi wahubiri wazembe," kasema "Mnaketi hapa huku mmeweka mguu wenu juu ya dawati na—na kuwapigia watu hawa simu badala ya kuwatembelea baada ya chakula cha jioni na kuzungumza nao."

298 Loo, moyo wangu ulikuwa ukiwaka moto. Nikawaza, "Ewe Mtu mashuhuri wa Mungu, ninachukia kutokubaliana nawe hapa, lakini hao wahubiri wavivu walikuwa ni akina nani kwa huyo mwongofu mmoja wa Paulo? Alivyofanya, alimchukua akamwingiza kwenye Neno, akamwingiza katika Ujumbe, akampeleka mpaka mahali ambapo alimpata Mungu; moyo wake ulikuwa unawaka moto, akawasha nchi moto! Na jambo tu unalofanya ni kuwaweka katika kanisa la Kibatisti ama la Kimethodisti, ama cho chote kile, si ajabu hakuna kitu cha kuwaka moto." A-ha. Naam, bwana!

299 Halafu angalia kile Neno lilichoahidi kwa ajili ya siku hizi. Hebu na tuone kama ni Methodisti, Batisti, Wapentekoste, ama ni kitu gani, kwa siku hizi. Sasa unaweza kwenda kusoma Maandiko yako. Uchukue Maandiko haya niliyokuwa nikiwanukulia. Pia Ufunuo...

300 Kama ningalikuwa na wakati, ningesoma hilo, lakini sina. Nina kama dakika kumi na mbili ama kumi na nne zaidi. Sina budi kufunga katika wakati unaofaa, kwenye saa tano, kama nikiweza.

301 Angalia Malaki 4, Ufunuo 10, Mihuri Saba. Je! si Biblia haikusema... Sasa angalia! Kulikuwako na Malaika, Mjumbe kutoka juu; na mjumbe wa duniani. Na kila mjumbe alikuwa ni kwa ajili ya wakati wa kanisa. Yeye alisema, "Katika siku..." akinena sasa, "alikuja malaika, mjumbe" (neno *malaika*, ni neno la Kiingereza linalomaanisha "mjumbe"). "...alishuka kutoka Mbinguni, akaweka mguu Wake juu ya nchi na bahari, akaapa kwa Yeye aliye hai hata milele ya kwamba hakutakuwa na wakati baada ya haya." Hiyo ni kweli? Upinde wa mvua juu ya kichwa Chake, na mambo yote haya yakitukia tu. Malaika huyo alikuwa ni Kristo! Bila shaka! Lakini Yeye alisema nini? "Lakini katika siku za malaika wa saba, wakati wa saba wa kanisa."

302 Sikuzote ni katika mwisho wa wakati wa kanisa kabisa ambapo wananinii mambo sana...mambo ya kanisa yamechafuliwa sana mpaka Mungu anamtuma mjumbe, na huo ni Ujumbe kwa wakati huo wa kanisa. Ndipo wanapokea

ujumbe wake, maana anaishi tu muda kidogo, na Mungu. . . ndipo wanachukua ujumbe wake badala ya kuuendeleza pamoja sehemu nyingine Yake, wanaunda ma—madhehebu. Ndipo wanakuja na kuunda madhehebu mengine; mjumbe mwingine, wanachukua mwingine.

303 Nyote mmeona katika kitabu changu, yote yataelezewa vizuri *katika Nyakati Saba za Kanisa,* jambo ambalo Yeye aliniambia; ambalo ninatetea kama shahidi kwa Mungu nitakayehukumiwa kwenye siku ya Hukumu kwa ajili Yake. Linatoka kwa Mungu, si kwenye mawazo yangu. Angalia, hapa. Niliwazia—niliwazia tofauti na hayo, kama nilikuwa nitumie mawazo yangu mwenyewe. Kama vile Ndugu Jack alivyoniambia juu ya Malaika pale, jinsi ambavyo "Huyo Kristo alikuwa ni mwili uliotukuzwa." Lakini sivyo, ilikuwa ikionyesha ya kwamba huo Ujumbe ulikuwa sahihi, Mungu Mkuu, Yeye alikuwa ni Mungu. Unaona? Ni kitu kile kile tu nilichokuwa nikihubiri kutoka kwenye Neno. Neno daima hushuhudia Neno.

304 Sasa, upesi sasa, tunapojitayarisha kufunga katika dakika chache.

305 Sasa, Yeye alisema, "Katika siku za Ujumbe wa malaika wa saba, malaika wa duniani, wakati wa saba wa kanisa, basi siri hizi zote ambazo zimepotezwa huko nyuma katika nyakati hizi nyingine sita za kanisa zitafunuliwa wakati uo huo." Vema, hivyo ndivyo hao Malaika walivyosema hasa. Hii hapa ile Mihuri Saba, ama kule kufunguliwa kwa siri hizi. Nawe jaribu kuzipeleka mbele ya hayo madhehebu. Kinyume na yale wao. . .Ndugu, wanafunga kama chaza, lakini daima wamefanya hivyo. Lakini ni majira yake!

306 Ni wangapi wanaojua ya kwamba huu ni wakati wa saba wa kanisa? semeni "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina!"—Mh.] Wakati wa Laodikia, ni vuguvugu ambao Mungu anatema kutoka kinywani Mwake. Nao wanamtema Mungu kutoka kinywani mwao; hakuna wakati mwingine katika Biblia ambapo Yesu alipakutwa nje akijaribu kubisha, apate kuingia. Walimfukuza nje, hakuna ushirikiano. Yesu ni nani? Neno! Neno lilitolewa nje. Makapi yalitupa ngano nje! Yeye alisema, "Ninasimama mlangoni na kubisha, na mtu ye yote katika pingu hizo huko nje atasikia Sauti Yangu." Ee Mungu, uturehemu.

307 Ilikuwa ndio wakati huo basi, wakati mtu huyo alipokufa, ambapo Daudi akiwa na upako alipoona kile alichokosea. Ee Daudi, ewe mchungaji, je! kuona kanuni zenu zilizokufa na madhehebu mnayoshikilia? Huwezi kuona kile yanachofanya? Yanawaua akina Uzia. Kufa kiroho, halafu mnashangaa kwa nini hakuna ufufuo; kuwaachilia wanawake wenu wakate nywele zao, wajipodoe, wavae suruali fupi; mnapeleka wavulana wenu kwenye shule za *kihuni*, na kadhalika namna hiyo, ambapo nusu yao wanarudi nyumbani wakiwa walawiti, na kila kitu.

308 Angalia kusudi la Daudi: alikuwa akileta lile sanduku nyumbani mwake *mwenyewe*. Hiyo haikuwa mji mkuu, si mahali penyewe, mahali pake palikuwa ni Yerusalemu. Lakini Daudi alikuwa akilileta nyumbani kwake *mwenyewe*, alikuwa anataka ufufuo uwe kwenye madhehebu yake mwenyewe. "Loo, kama wewe ni wa Assembly, sawa. Kama wewe ni wa Umoja, vema. Kama wewe ni Mpentekoste, sawa."

309 Kama vile mtu fulani alivyosema, alisema, "Ndugu Branham, unapataje mtu wa kukusikiliza?" Kasema, "Ninaweza kumwona Billy Graham, yeye anaungwa mkono na kila madhehebu nchini. Ninaweza kumwona Oral Roberts, kila Mpentekoste anamuunga mkono moja kwa moja. Lakini," kasema "wewe unapinga kitu kizima." A-ha. Kasema, "Unapataje mtu ye yote basi?"

310 Nikasema, "Ni Mungu!"

311 "Mimi Bwana nimelipanda kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Nitalitia maji mchana na usiku asije mtu akalitoa mkononi Mwangu," Isaya. "Nitalitia maji, nililipanda. Niliandika majina yao katika Kitabu kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, kwa kuchaguliwa tangu zamani. Nitalitia maji, endelea tu kusonga mbele. Nitatoa maji, wewe linyunyizie tu." Kweli. Unaona? "Nitalitia maji usiku na mchana asije mtu akalitoa kutoka katika mkono Wangu." Haya basi.

312 Alitaka lije kwenye mji wa Daudi, mji wa Yerusalemu. Hapakuwapo na mahali palipokuwa tayari kwa ajili yake wakati huo, na ndivyo ilivyo siku hizi. Siri hizi kuu ambazo zimefunuliwa na Mihuri Saba, hakuna mahali katika madhehebu yo yote. . . itakubidi kuyaacha madhehebu upate kuzikubali. Kote kote kutoka kwa Luther hata kufikia kwa Umoja wa Kipentekoste, hakuna mahali panapoweza kulipokea. Wala mwanadamu hawezi kulipokea na abakie katika madhehebu yake. Itambidi kufuata ngano la sivyo aende pamoja na kapi, achague mojawapo.

313 Kristo ndiye Sanduku letu, Neno. Wao wanataka madhehebu yao. Hawezi, angalia, hawezi kubebwa juu ya magari mapya ya madhehebu, Ujumbe Wake hauwezi kwenda kwenye gari la madhehebu mapya wakati linapopaswa kubebwa na kuja kwenye moyo wa nabii. Hauwezi. Yeye aliahidi jambo hilo, lingekuwa namna hiyo, na hivyo ndivyo inavyopaswa kuwa.

314 Kwa hiyo madhehebu hayatalipokea kamwe, wala hayawezi kulipokea. Nayo ni vipofu kwa hilo kama vile Wayahudi walivyokuwa walipomsulibisha Yesu msalabani, wakati Yesu aliposema, "Baba, wasamehe, hata hawajui watendalo." Usiwadharau, lakini omba tu. Kwa kuwa vipi kama wewe ungalikuwa katika hali ile ile na macho yako ni yamepofuka sana hata huwezi kuamka na kuona kinachoendelea?

315 Wala hawangeweza kuona ya kwamba huyo alikuwa ndiye Mungu wao hasa. Wakati alipokuwa amening'inia pale msalabani, na wao wakiimba Zaburi 22 hekaluni, kwenye umbali wa yadi mia mbili, "Mungu Wangu, Mungu Wangu, mbona umeniacha? Walichoma miguu Yangu na mikono Yangu." Unaona? "mifupa yangu yote, inanikodolea macho. Mbona umeniacha?" Na hapo, Mungu yeye yule waliyekuwa wamemwimbia, walikuwa vipofu kutosha hata wakamwangika kwa misumari msalabani, wala hawakujua.

316 Sasa, hivi Biblia haisemi ya kwamba kanisa la Laodikia, ambalo linafikiri ya kwamba ni kubwa sana kwa wafuasi wake wa kimaedhehebu, litakuwa "uchi, lenye mashaka, maskini, kipofu, wala halijui"? Maana ya *Kipofu* ni nini? *Kipofu* linamaanisha kwa kanisa hili la Laodikia kama lilivyomaanisha kwenye mwisho wa kanisa la Kiyahudi, ni kipofu kwa Kristo yeye yule waliyemweka nje, akigonga mlango, akijaribu kuingia ndani; "uchi, lenye mashaka, maskini, nyonge, kipofu, wala halijui." Ee Mungu wa rehema!

317 Kwa nini ngano isikae katika Uwepo, yule Mwana wa Nuru, kuona saa tunayoishi? Naam, Kristo ndiye Safina yetu, lakini njia Yake ya asili ya kufanya jambo hilo. Basi huyu hapa . . . Walikuwa na Roho wake kweli, tunajua hilo. Wanamngojea Bwana, wanaona mpango Wake juu ya Neno Lake la asili katika majira yake kuthibitishwa, hivyo ndivyo tunavyopaswa kuwa tukifanya sasa hivi. Naye ana—anafunua imani yao kwa Neno Lake, wakimwona akithibitisha kila mpango ambao Yeye aliahidi, si mipango ya kibinadamu ya madhehebu, si kufanya wafuasi kwa ajili ya safina yetu.

318 Wao wana safina ya Kimethodisti, safina ya Kibatisti, safina ya Kipresibiteri, kila mtu anaingia kwenye safina hii kwa ajili ya ile dhiki kuu inayokuja; "Utukufu kwa Mungu! Nilibatizwa katika safina ya Kimethodisti, ya Kipresibiteri, ya Kipentekoste." Kuna safina moja tu, hiyo ni Yesu Kristo, Naye ni Neno!

319 Angalia, Mungu alimwambia nabii, akasema, "Kula hilo gombo," katika Agano la Kale. Nabii wa Agano Jipya, Yeye alisema, "Kula hicho kitabu kidogo." Kwa nini? Kusudi nabii na Neno wawe mmoja! Unaona? Hiyo ndiyo Safina, Neno la Mungu.

320 Mungu ameahidi Neno Lake, jinsi ambavyo lingetimizwa na jinsi lingetimia wakati alipomchagua Bibi-arusi Wake, jinsi lingetendeka. Hilo linatendeka moja kwa moja mbele yenu, katika Jina la Bwana, na hilo ni kwa Neno la asili! Ujumbe wa wakati wa jioni uko hapa.

321 Ni wangapi wanaomkumbuka Haywood wakati alipoandika:

> Kutakuwako Nuru kwenye wakati wa jioni,
> Njia ya Utukufu hakika mtaipata.

322 Naam, ile ahadi ya jioni ya Mihuri Saba, ya Ufunuo 10, Malaki 4, Luka 30 na 10. Soma Kumbukumbu la Torati 4, 4:1 na 4, halafu kifungu cha 25 na 26, uone vile alivyosema kuhusu siku hii ya mwisho. Hii ilikuwa ni Musa akiwaambia Israeli "Kuweka kila Neno, usiongeze jambo moja!" Musa, nabii huyo alikuwa amepanda kule juu na kuona Neno Hilo la Mungu. Nalo liliandikwa kwa ajili yake na kuthibitishwa kwa kuandikwa na mkono wa Mungu Mwenyewe. Akasema, "Tiini kila Neno, msiongeze jambo moja Kwake wala kuondoa jambo moja Kwake." Unaweza kusoma hayo katika kifungu cha 25 na cha 26 cha Kumbukumbu la Torati 4.

323 Angalia! Usiongeze Kwake, usitoe Kwake; maana kama ukitoa, Mungu atakuondolea sehemu yako katika Kitabu cha Uzima. Na inaonyesha ya kwamba wewe hukuwa ni mbegu Yake."

324 Kumbuka! Kila kitu ambacho Mungu ametuahidi, kila kitu ambacho Mungu amesema nasi, kila kitu ambacho umeambiwa katika Jina la Bwana, kimetukia! Mungu kamwe hajaghairi ahadi moja, lakini Yeye ametimiza kila ahadi aliyosema, aliyotuambia, imekuwa ni Kweli kwa miaka hii ishirini, Shreveport. Nimewahubirini katika nguvu za Mungu, na kwa heshima ya mchungaji wenu, nami nawakumbusha leo. Hata wanawake waliopita umri wa kuzaa; wanaume, watoto, mateso, kuponya, kutoa unabii, mambo ambayo yangetukia, hakuna hata moja limeshindwa! Sasa, kaeni mbali na hayo madhehebu, yanawaongoza mautini.

325 Samweli alisimama siku moja, nao wakasema, "Tunataka mfalme, tunataka kuwa kama watu wengine wa ulimwengu."

326 Vema, Samweli akasema, "Msikubali kuwa na huyo mfalme. Atawachukua wana wenu, na binti zenu, na atafanya *hivi* na atafanya *vile*."

327 Akasema, "Naam, ninajua mnasema kweli."

328 Lakini Samweli akasema, "Nisikilizeni mimi. Je! niliwahi kuchukua pesa zenu zo zote? Je! niliwahi kuwaomba riziki yangu? Je! niliwahi kuwaambia mnapaswa kunipa kiasi fulani cha mshahara kusudi niwafanyie mkutano?" Sasa amueni ninyi wenyewe, hata sasa! Unaona? Akasema, "Je! niliwahi kuwaambia cho chote katika Jina la Bwana ila kile kilichotimia?" Hata kitu kimoja.

329 "Loo, naam, Samweli, kamwe hujatuomba pesa, hujakuwa na shauku ya mambo makubwa. Samweli, hiyo ni kweli, na kila kitu ulichotuambia katika Jina la Bwana kilitimia. Lakini, Samweli, tunatata madhehebu yetu hata hivyo!"

330 "Basi nendeni mkayachukue. Ni juu yenu." Hiyo ni kweli.

331 Unaweza kufikiri unamtumikia Mungu, na endapo unatoka nje ya njia ya Mungu ya kufanya jambo hilo, utaendelea

kuvuruga mambo, zaidi na zaidi. Ee kanisa la Mungu aliye hai! Samahani kwa njia yangu ya Kiairishi na ucheshi wangu, lakini katika unyofu na unyenyekevu wa moyo wangu, ninyi Assemblies of God, ninyi Oneness, Wapresbiteri, Wamethodisti, cho chote mlicho, kimbieni kuokoa maisha yenu. Kumbukeni, tokeni humo.

Mataifa yanavunjika, Israeli inaamka,
(ikijitayarisha kwa ajili ya yule aliyesalia)
Ishara walizotabiri manabii;
Siku za kimadhehebu zimehesabiwa
zimekumbwa na dhiki,
Rudini, enyi mliotawanyika, makwenu.

Siku ya ukombozi imekaribia,
Mioyo ya wanadamu inazimia kwa hofu,
Jazweni na Roho Wake,
Taa zenu na zitengenezwe na kusafishwa,
Angalieni juu, ukombozi wenu unakaribia.

332 Je! unaamini jambo hilo? Tuko katika wakati wa mwisho, tumewasili. Maandishi ya mkono yako ukutani, kuja kwa pili kumekaribia, Bibi-arusi anachaguliwa, na kumwagiliwa maji, anatolewa.

333 Sasa, hiyo haimaanishi kutolewa kanisani, hiyo inamaanisha kutolewa atoke kwenye umadhehebu. Lazima uende kanisani, lakini usijiunge na madhehebu yo yote. Yesu alienda na madhehebu yote, bali hakujiunga na hata moja la hayo. Wala hakuungana na hata moja la hayo, la hasha, lakini alikuwa miongoni mwao. Huko ndiko Nuru inakopaswa kuangazwa. Na unakaa mahali ulipo ukiangaza Nuru. Unaona? Mungu anakutumia kwa ajili ya hiyo. Watu wenye njaa, hebu waache waone ya kwamba Yesu Kristo ni halisi, sawasawa na alivyokuwa jana, ndivyo alivyo na leo; na atakuwa milele.

334 Inawezekana ya kwamba mwanamume ama mwanamke kwa unyofu wote, wakijaribu wawezavyo kumtumikia Mungu, na kuichochea kwa njia mbaya. Wakiwa na upako halisi wa Roho Mtakatifu juu yao, lakini wanaichochea kinyume cha mpango wa Mungu kwa ajili ya wakati huo, na kuvuruga jambo zima. Sasa, kama unaamini ya kwamba hiyo ni Kweli, sema, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina!"—Mh.] Ndio kwanza tulisome Hilo. Wakavuruga jambo hilo lote kwa kutokuja kwa njia iliyoandaliwa na Mungu ya kufanya jambo hilo.

Na tuombe:

335 Ee kanisa, hapa na kote nchini, sikilizeni mtumishi wenu mnyonge asubuhi ya leo. Je! mtafanya hivyo? Angalieni mahali mlipokuwa miaka michache iliyopita wakati huu kwanza ulipoanza; sasa angalieni ni maigizo gani yameutumia kwa faida yao, na mamilioni na mabilioni ya dolla chungu nzima yamemiminika kwenye madhehebu. Unaona? Bado wangali

mbali na Neno la Mungu. Mungu hachochei Roho Wake kwa majengo na madhehebu. Yeye humchochea moja kwa moja katika Neno Lake, kulifanya liishi. Na kama ulichaguliwa tangu mwanzo wa dunia kwenye Neno hilo, kila Neno litakuja moja kwa moja juu ya Neno. Kama vile seli ya mwanadamu haitakuwa na seli moja ya mwanadamu, na seli nyingine ni ya mbwa, na inayofuata ni seli nyingine ni ya paka; zitakuwa ni seli za binadamu. Lakini huna budi kuwa na seli kwanza. Hiyo ni kweli? semeni, "amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."— Mh.] Vema, kama ni seli ya Neno kwa kuanzia, hizo seli zingine za Neno zimechaguliwa kuufanya mwili mzima.

336 Msiwe watoto, isipokuwa tu katika upendo, lakini mwe watu wazima katika Roho na uamuzi. Amueni kama nimewaambia Kweli ama la. Amueni kama Hilo ni Neno la Mungu ama silo. Amueni kama hii ndiyo saa tunayonena habari zake ama siyo. Amueni kama mambo haya yameahidiwa. Sasa, je! yamethibitishwa? Kwa mambo ambayo hakuna mwanadamu duniani angeweza kufanya. Lakini yamekuwa ya kwaida sana kwetu mpaka tunayaacha yatupite moja kwa moja. Kesheni, kanisa, kesheni.

337 Kama kuna mmoja hapa asubuhi ya leo ambaye hamjui Yesu Kristo, hajahesabiwa haki asubuhi ya leo, dhambi zako zote zimeondolewa kama kwamba hukuwa umetenda dhambi kamwe, na unataka kuwa namna hiyo. . . maana kumbuka, siku moja, huenda ikawa ni leo, labda katika dakika tano zijazo, lakini siku moja moyo huo utasimama. Na hiyo ndani ya ndani itaruka iende ikasimame mbele ya uwepo wa Mungu ikahukumiwe kulingana na kile unachofanya na Ujumbe huu asubuhi ya leo, kulingana na Ujumbe *huu* ambao unaona. Si . . . Si mimi, mimi ni kinywa tu. Kama mikrofoni hii, haiwezi kusema neno nisipozungumza ndani yake. Wala mimi nisingeweza kusema cho chote Mungu asipozungumza katika hilo, lakini unaona Mungu ameuthibitisha kwamba ni Kweli. Inatakiwa uwe Mkristo halisi.

338 Sasa, hatuna mahali pa wito wa madhabahuni, lakini papo hapo mezani mahali unapoketi. Mahali hapa pamejaa watu na kusongamana, kufurika. Nisingeweza kuwaita kwenye madhabahu, hakuna madhabahu hapa ya kuwaitia. Bali madhabahu iko moyoni mwako. Ruhusu ushawishi huo mdogo ya kwamba "Yesu Kristo ni halisi" usogee karibu sana leo na kuita Mwili wake mwingine kwako, upate kumweka kwenye hori la moyo wako? Kama hayuko humo, tafadhali inua mkono wako, na umpungie mkono, ukisema, "Bwana, nijaze, nijaze kwa Neno Lako na kwa Uwepo Wako, kusudi nipate kuishi Kwako"?

339 Wakati kila kichwa kimeinamishwa, kila jicho limefungwa, kila mahali nchini, inueni mikono yenu hapa katika wasikilizaji wanaoonekana na huko nje pia; nami nitawaombea. Hivyo tu ndivyo ninavyoweza kufanya, siwezi kuijaza. Mungu akubariki.

Siwezi kuijaza. Mungu akubariki; na wewe. Mungu anaweza kuijaza. Mungu akubariki. Mikono inainuliwa hapa katika wasikilizaji wanaoonekana, kila mahali. "Ijaze. Nijaze, Ee Bwana. Nijaze." Na sasa, baada ya mimi . . . Asante dada. Asante ndugu. Baada ya mimi . . . Mungu akubariki, Mungu akubariki, dada mpendwa. Wewe. Baada . . . Nafikiri sasa nimeshika karibu wote wa walio waaminifu sana, wanaojaribu kuwa, ninataka kuinua mikono yangu pamoja nanyi.

340 Ee Bwana, usiniache katu nifikie mahali pa kusimama. Sikuzote, Bwana, jalia nisisimame kwenye jambo moja, jalia nisonge mbele tu, Bwana, mpaka nitakapomaliza kila kitu ambacho Wewe ulikusudia nikifanye. Haidhuru gharama yake ni nini, haidhuru itagharimu nini, bila kujali lawama, jinsi msalaba ulivyo mgumu, nitakumbuka msalaba uliobeba.

> Kwa hiyo huu msalaba uliowekwa wakfu nitaubeba
> Mpaka kifo kitakaponiweka huru;
> Kisha niende nyumbani, nikavae taji,
> Kuna taji kwa ajili yangu.
>
> Je! Yesu ubebe msalaba peke Yake,
> Na ulimwengu wote uwe huru?
> La, kuna msalaba kwa ajili ya kila mmoja wa wana Wake,
> Kuna msalaba kwa ajili yangu.

341 Mungu mpendwa, Neno limehubiriwa. Haliwezi kurudi bure, litapata mahali pake mahali fulani. Kama mbegu imepandwa tayari, litaitia maji mpaka ikue. Wala hakuna mtu anayeweza kuitoa katika mkono Wako, "Wote alionipa Baba watakuja Kwangu, hakuna mtu anayeweza kuwatoa kwenye mkono Wangu. Baba amenipa hao kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu"; wakati mipango yote ilipoandaliwa, basi, Yesu apewa Kanisa Lake, Bibi-arusi Wake.

342 Arusi ya bandia ya ulimwengu, kwa haya madhehebu. Wewe ulikuja na ukafa ulimwenguni, ukamkomboa, ukamhesabia haki, kwanza hakutenda hayo. Alinaswa katika mambo hayo, kipofu. Na kama ule wimbo unavyosema:

> Wakati mmoja nilikuwa nimepotea na sasa nimepatikana,
> Wakati mmoja nilikuwa katika Laodikia, kipofu, lakini sasa naona.
>
> Na ni neema iliyoufundisha moyo wangu kuhofu,
> Neema ndiyo iliyoondoa hofu yangu;
> Jinsi hiyo neema ilivyoonekana ya thamani
> Ile saa niliyoamini mara ya kwanza.

Na maji ya Mungu iliingia nafsini mwangu. Nilikuwa ninakauka.

343 Mungu, kwenye madhabahu hii ndogo ya kila moyo uliopo hapa na kote nchini, naomba maji yanayotoka chini ya madhabahu ya Mungu na yabubujike asubuni ya leo juu ya Kanisa; na kulimwagilia maji, Bwana, kwa majira yaliyo karibu kuisha. Lipe Uzima, Maji ya Uzima, lipate kukaa katika Uwepo wa yule Mwana kusudi iivishwe kwa ajili ya ghala Lako kuu.

344 Baba, ninawaombea. Lakini ubua hauna budi kukauka, kwa hiyo siwezi kuuombea; hauna budi kufa, kwa hiyo umekufa. Lakini ninaiombea ngano, Bwana, inayoumbika Mwili wa Kristo. Tujalie, Bwana, ya kwamba maji baridi ya Mungu yatadumisha mashavu yake masafi na maji ya furaha na ufahamu mpaka kivuna nafaka kitakapokuja kuipeleka Nyumbani. Katika Jina la Yesu, ninalikabidhi lote Kwako, Bwana; matokeo ni Yako. Amina.

345 [Dada mmoja katika kusanyiko anatoa ujumbe—Mh.] Amina.

346 Kwa hiyo Baba, Mungu, tunakushukuru. Na, Baba, tunamwombea dada yetu mdogo, mjakazi hapa, apate nguvu zake. Ninafikiria wakati ambao wakati ni—nilipotembea mbele yake, jinsi ambavyo Roho alikuja juu yake na kutoa ujumbe ule ule ambao Malaika wa Bwana alitoa Mtoni siku hiyo: "Kama vile Yohana Mbatizaji alivyotumwa kutangulia kuja kwa kwanza kwa Bwana Yesu, wewe umetumwa kutangulia kuja mara ya pili."

347 Tunapoona ikiumbika sasa kufikia sehemu ya ngano, Mungu, tunakushukuru kwa ajili ya kila kitu ambacho umefanya. Mioyo yetu imejazwa isivyosemeka. Ninajisikia nimejaa sana, Bwana, sijui kabisa jinsi ya kusema cho chote kile. Bali nakushukuru Baba, tena, kwa yote yale uliyotufanyia. Katika Jina la Yesu Kristo.

> Nampenda, . . .

Hebu tumwimbie tu, sasa. Kumbukeni, Yeye yuko hapa.

> Kwani alinipenda kwanza,
> Na kununua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.

348 Je, hilo linawafanya mjisikie duni sana, duni sana? Mmemwaga yote, mkiwa tayari kwa Roho, unaona.

> Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
> Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
> Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele,
> Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!

> Usitamani utajiri wa batili wa dunia hii,
> Unaooza upesi sana,
> Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele,
> (hakuna madhehebu, sasa)
> Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!

Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele,
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!

349 Ni wangapi wanaojaribu kufanya jambo hilo? Inua mkono wako. Sasa nyosha mkono wako upande wa pili wa meza, shikaneni mikono, namna hii. Kwa pamoja . . . Mnaweza kuketi, hilo ni swa, ama cho chote mnachotaka kufanya. Sikilizeni kwa makini. Hebu na tuuimbe kwa pamoja sasa. Hii inawakilisha mnyororo wetu usiovunjika wa upendo wa Mungu. Tunashikana mikono sisi kwa sisi kwa sababu tunamwamini Mungu. Tunagusana sisi kwa sisi kwa sababu sisi ni ndugu na dada, Roho yule yule anayetutuma, Neno la Milele la Mungu likiishi mioyoni mwetu akidhihirishwa.

Safari yetu itakapokwisha,
Kama tumekuwa waaminifu kwa Mungu,
Maskani yetu Utukufuni yatakuwa mazuri na yanayong'ara,
Nafsi yetu iliyojaa furaha itayaona!

Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele,
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika! (Roho wa Bwana!)

Shikilia Mkono wa Mungu . . .

Weka tu moyo wako Kwake, unaona. Mikutano kama hii ndiyo unayopaswa kuhudhuria wakati ujao.

. . . usiobadilika!
Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele (Neno pekee ndilo la Milele)
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!

Usitamani kupendwa na watu, elimu ibatilikayo ya ulimwengu,
Inayooza upesi, (Iangalie siku hizi, vile ilivyofanya)
Tafuta kupata hazina ya mbinguni,
Hazitapita kamwe!

Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele,
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!

350 [Dada fulani anatoa ujumbe katika lugha, Ndugu Branham anaanza kuuvumisha huo wimbo *Shikilia Mkono wa Mungu Usiobadilika*. Dada mwingine anatoa tafsiri yake—Mh.]

351 Jinsi tunavyokushukuru, Bwana. Tunapoketi katika wakati huu wenye uchaji, karibu kama kwenye mazishi, kwa

maana tunakabili mazishi ya ulimwengu uliokufa, ulimwengu unaokufa; kanisa linalokufa, lililokufa.

Ee Mungu, kusanya ngano Yako haraka, Baba. Njoo upesi, Bwana Yesu.

352 Bariki watu wako, Baba, leta uaminifu na kilindi kwenye mioyo ya watu. Jalia tutoke kwenye hayo madansi dhaifu na batili, tutulie kwenye utajiri mkubwa wa asali ya Mungu. Tujalie, Bwana. Weka mioyo yetu imara kwa upendo na uaminifu.

353 Wabariki watu Wako kila mahali, Baba. Tunapoondoka mahali hapa jalia twende katika Jina la Bwana Yesu tukazungumze yale yaliyo manyofu, yale yaliyo ya Kweli, yale yaliyo sawa, jalia tuache yale yaliyo mabaya, Bwana. Wakati mtu anapoanza kutudanganya, na tumwonyeshe kisogo upesi, tukatae mizaha yote michafu, mibaya na mambo ya ulimwengu, na tuyape kisogo tu na kujiondokea. Tusaidie, Mungu mpendwa. Tufinyange, tutengeneze, tuvunje, na utufanye kuwa mfano wa wana na binti za Mungu tupate kutenda kazi kwa nguvu za Roho Mtakatifu. Tunajikabidhi Kwako, huku tumeshikana mikono, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Hebu na tusimame. Ndugu Noel.

*KUJARIBU KUMTUMIKIA MUNGU BILA YA KUWA NI MAPENZI YA MUNGU* SWA65-1127B
(Trying To Do God A Service Without It Being God's Will)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumamosi asubuhi, 27 Novemba, 1965, katika Washington Youree Hotel kule Shreveport, Louisiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Hii tafsiri ya Kiswahili ilichapishwa mwaka wa 2003 na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2003 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org